CHUO KIDOGO CHA BIBLIA

MAHUBIRI YA MLIMANI
Uchambuzi Mstari Kwa Mstari
(Mathayo Sura Ya 5, 6 Na 7)

KIJITABU CHA KUJIFUNZIA CHA THELATHINI NA TATU

ORODHA YA YALIYOMO

UTANGULIZI 3

"FARAGHA YA KWANZA YA KIKRISTO" 3

SURA YA KWANZA 6

YALIYOMO KATIKA MAHUBIRI YA MLIMANI 6

"Hali Za Moyo Zinazokuja" 6

Hali Za Moyo Zinazofanya Mtu Aje 8

SURA YA PILI 20

"HALI ZA MOYO ZINAZOSABABISHA KWENDA" 20

SURA YA TATU 27

"KOBE KWENYE NGUZO" 27

SURA YA NNE 33

"HAKI YENYE KUHUSIANA" 33

SURA YA TANO 50

"NIDHAMU KIROHO NA THAMANI ZA JUU" 50

MAMBO YENYE THAMANI YA JUU KWA MWANAFUNZI 59

SURA YA SITA 63

"MWALIKO" 63

Utangulizi

“Faragha Ya Kwanza Ya Kikristo”

(Mathayo 4:23 hadi 5:1)

Watu wengi, hata wasiojifanya kuwa wafuasi wa Kristo, wanakubali kwa mdomo mafundisho ya Yesu Kristo yapatikanayo katika “Mahubiri Ya Mlimani”. Wasomi, wanasiasa na hata watunga mashairi wamekuwa wakitumia baadhi ya mafundisho Yake bila hata ya kumjua Yeye aliyeyatoa. Pengine hakuna fungu lingine katika Biblia linalotajwa sana na kueleweka kidogo sana, kuliko fundisho hili la Yesu ambalo tunakwenda kujifunza wakati huu.

Mantiki Ya Mahubiri Yenyewe

Ni muhimu kuona mantiki kabla ya kutazama yaliyomo katika mafundisho haya maarufu. Tunapata maelezo ya mantiki ya mahubiri haya wakati Mathayo anaposema hivi:

“Yesu akapita katika Galilaya, akifundisha kwenye masinagogi yao, na kuhubiri habari njema za ufalme na kuponya kila maradhi na magonjwa yaliyokua katika watu. Habari Zake zikaenea Shamu yote. Watu wakamletea waliokuwa na magonjwa mbalimbali, na waliokuwa na maumivu makali, na wenye pepo, na waliokuwa na kifafa, na waliopooza, akawaponya wote. Makundi makubwa ya watu kutoka Galilaya, na kutoka ile Miji Kumi, na kutoka Yerusalemu, na kutoka Uyahudi wote na maeneo ng’ambo ya Yordani walimfuata.

“Naye alipoona makundi hayo ya watu, alipanda juu ya mlima, na alipokwisha kuketi, wanafunzi Wake walimjia. Kisha akafungua mdomo Wake na kuanza kuwafundisha, akisema hivi …” (ktk Mathayo 4:23 hadi 5:1, TLR).

Ndipo tunaposoma sura ya tano, ya sita na ya saba katika Injili ya Mathayo, ambapo kuna mafundisho haya ya ajabu sana aliyotoa Yesu huko. Je, sasa unaweza kuelewa mantiki ya kutolewa mafundisho haya maarufu? Tunaweza kuyaita “Faragha Ya Kwanza

Ya Kikristo". Haya hayakuwa mahubiri kwa maana ya mahubiri siku hizi, bali ni mafundisho yaliyotolewa na Yesu, katika hali tunayoweza kuiita faragha, iliyofanyikia mlimani.

Yesu alipomaliza huduma Yake ya miaka mitatu kwa watu wote, alitumia masaa Yake ya mwisho katika chumba cha juu akiwa na mitume aliokuwa amewakusanya na kuwafundisha, kabla ya kukamatwa Kwake na hatimaye kufa msalabani. Huko alizungumza nao kwa kirefu, na mafundisho hayo tunayaita "Faragha Ya Mwisho Ya Kikristo" ambayo Yesu alifanya na wanafunzi Wake (ktk Yohana sura ya 13 hadi 16).

Tumetaja maelezo ya Mathayo yanayohusu mantiki kwa ajili ya hii Faragha Ya Kwanza Ya Kikristo. Yesu alikuwa anaponya kila aina ya ugonjwa miongoni mwa watu hao waliokuwa wamekusanyika kando-kando ya vilima vilivyozunguka Bahari Ya Galilaya. Kulingana na Mathayo, hao watu walikuwa "… na magonjwa mbalimbali, na wenye maumivu makali, na wenye pepo, na wenye kifafa, na wenye kupooza, Naye akawaponywa wote" (ktk Mathayo 4:24, TLR).

Tunasoma pia kwamba hao waliokuwa wamekusanyika kando ya Bahari ya Galilaya, walikuwa wamesafiri "… kutoka ile Miji Kumi, na Yerusalemu, na kutoka Uyahudi, na maeneo ya ng'ambo ya Yordani" (ms. 25, TLR). Palikuwa na safari ya kama siku nne hivi kutoka ng'ambo ya Jordani hadi kufika Galilaya, mahali ambapo Yesu alikuwa anaponya hao wagonjwa.

Leo hii katika tamaduni zetu nyingi, matatizo kama hayo yanashughulikiwa kwa wahusika kuwekwa mahali: wagonjwa na wanaokaribia kufa, wenye matatizo ya akili, wazee na waliojeruhiwa katika vita zetu. Watu aina hiyo hufichwa mahali, na hata kusahauliwa kabisa. Wakati Yesu alipopanga faragha Yake, matatizo hayo yote tuliyotaja hapo yalikuwepo katikati ya watu waliokuwa wamekusanyika kandokando ya Bahari Ya Galilaya.

Ukifanikiwa kwenda kusomea shahada katika vyuo au ukipata nafasi ya kuhudhuria semina kuhusu jinsi ya kuwa mtendaji mzuri, utaambiwa kwamba inabidi ujifunze jinsi ya kuchanganua, kupanga, kugawa kazi, kusimamia na halafu kuugua!

Yesu alichagua kutowaponya watu hao wote. Aliwakaribisha baadhi ya wanafunzi Wake kukutana Naye kwenye kilima kilichokuwa juu zaidi, karibu na kilele cha vilima vinavyozunguka Bahari ya Galilaya (ktk Marko 3:13). Tendo hilo liligawa makundi hayo ya watu kuwa mawili: waliokuwa chini ya kilima ni wale waliokuwa sehemu ya tatizo. Waliokuwa juu ya kilima pamoja na Yesu ni wale waliotaka kuwa sehemu ya Jibu Lake kwa matatizo yote yaliyokuwa chini ya kilima.

Yesu alitambua kwamba kwa kuwa alikwisha kubali mipaka itokanayo na kuwa na mwili wa kibinadamu na muda mfupi aliokuwa nao hapa duniani, asingeweza kutatua matatizo yote hayo akiwa peke Yake. Basi, "alichambua" ingawa tunajua kwamba ulikuwa ndiyo mpango Wake tangu mwanzo, wa kutumia wanadamu dhaifu kama sehemu ya Mpango Wake Mkuu. Kisha, akapanga hii Faragha ya Kikristo ya Kwanza. Marko anaandika kwamba Yesu aliwakaribisha wale waliohudhuria hii faragha "kuwa pamoja Naye, kisha awatume" (ktk Marko 3:13, 14, TLR).

Jinsi Yesu alivyopanga faragha hii, changamoto aliyokuwa anatoa ilikuwa hii: "Je, wewe ni sehemu ya tatizo au ni sehemu ya ufumbuzi wake?" Mkakati wa Yesu ulikuwa kuwaonyesha wale wote waliohudhuria faragha Yake jinsi ambavyo wangeweza kuwa sehemu ya ufumbuzi wa matatizo yote yale ya maishani, yaliyowakilishwa na waliokuwa chini ya kilima.

Yohana anataja kwa ufupi sana mantiki ya faragha hii. Anaandika kwamba wakati makundi makubwa ya watu yalipokuwa yanamjia Yesu kwa ajili ya uponyaji, Yeye aliketi kwenye kilima na wanafunzi Wake (Yohana 6:1-3). Yohana aliandika Injili yake miaka mingi sana baada ya Injili ya Mathayo na ya Marko. Bila shaka alikuwa anafahamu yaliyoandikwa na Mathayo, lakini yeye alikuwa na mkazo mwingine. Basi, hakufafanua sana mantiki ya mahubiri hayo. Mathayo ndiye anayetupa maelezo zaidi kuhusu mantiki ya Mahubiri ya Mlimani, pamoja na yaliyomo.

Msomi mmoja anajumuisha mantiki ya mahubiri haya maarufu kwa kutuambia kwamba Yesu anatoa kweli tatu muhimu sana anapoandaa mantiki kwa ajili ya mahubiri haya maarufu.

Wakati Yesu anapowaita wanafunzi kutoka katika hilo kundi kubwa la watu ili wawe sehemu ya Jibu Lake, tunaona kinachohusika katika kuwa Mkristo. Zile Heri nane anazotaja ni mahubiri na huonyesha picha ya hali inayohusika mtu kuwa Mkristo. Ile mifano minne inayokuja baada ya zile Heri, pamoja na mafundisho mengine yote katika sura ya tano, ya sita na ya saba, huonyesha changamoto inayotokea wakati tabia ya Kikristo inapogusa au kukutana na utamaduni usiokuwa wa Kikristo.

Baada ya utangulizi huu mfupi, hebu kwa pamoja tuingie katika Neno la Mungu na kuliruhusu lituingie. Hebu na tujifunze Mahubiri haya ya Mlimani kwa sababu yatabadilisha maisha yetu kama yalivyofanya kwa wale waliosikia siku ile, kisha wakaenda na kuipindua dunia yao.

Sura Ya Kwanza

Yaliyomo Katika Mahubiri Ya Mlimani

"Hali Za Moyo Zinazokuja"

(Mathayo 5:3-6)

Yesu Kristo alitoa mahubiri haya akiwa mlimani huko Galilaya, na katika mahubiri yenyewe aliwapa watu changamoto, wale waliodai kuwa ni wafuasi Wake, ya kusimama katikati ya upendo wa Mungu na maumivu ya watu wanaoteseka hapa duniani. Aliwahimiza wanafunzi Wake kumwunga Yeye mkono na kuwa njia za kupitisha upendo Wake. Akamalizia mahubiri Yake kwa kutoa mwito wenye nguvu sana kwa watu wajitoe na kujikabidhi Kwake. Kisha akachagua watu kumi na wawili waliosikia mahubiri Yake ili wawe "mitume" Wake, au, "watu waliotumwa". Hao mitume waliishi na kufa kwa ajili ya Yesu, walipozunguka dunia nzima na kuwafanya watu kuwa wanafunzi Wake.

Kwa kuwa tumekwisha tazama mantiki, tuko tayari sasa kutazama yaliyomo katika mahubiri haya maarufu sana. Tunasoma hivi: “Akafungua mdomo Wake na kuanza kuwafundisha, akisema hivi: ‘Wamebarikiwa walio maskini katika roho, kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao. Wamebarikiwa wanao-omboleza, kwa sababu watafarijiwa. Wamebarikiwa walio wapole, kwa sababu watairithi nchi. Wamebarikiwa wenye kuona njaa na kuwa na kiu kwa ajili ya haki, kwa sababu watajazwa’.” (5:3-6, TLR).

Yesu anaanza kwa kuwafundisha wanafunzi Wake hali nane za moyo – “zilizobarikiwa”. Yesu anaahidi kumbariki kila mwanafunzi mwenye hali mojawapo. Neno hili “amebarikiwa” linaweza pia kuwa na maana ya “ana furaha” au “amefanikiwa kiroho” au “mwenye neema”. Kila hali ya moyo moja pia ina ahadi inayoeleza jinsi baraka hiyo itakavyokuja katika maisha ya huyo mwanafunzi.

Hizi hali nane za moyo – hizi baraka – ni picha ya mtazamo wa mwanafunzi wa Yesu. Mantiki ya mafundisho haya inaonyesha kwamba huo mtazamo wa maisha utawafanya wanafunzi Wake kuwa sehemu ya ufumbuzi na jibu la Kristo kwa mateso yote duniani, yanayowakilishwa na kundi la watu walioko chini ya mlima.

Sisi kama wanafunzi wa Kristo, tunapoamua kwamba tunataka kuwa sehemu ya jibu na kuacha kuwa sehemu ya tatizo, kitu cha kwanza tunachotakiwa kufanya ni kujifunza hali hizi za moyo mpaka tuzielewe, kisha tufanye uamuzi wa kuishi kulingana na hizo kila siku ya maisha yetu. Kumbuka – kama tulivyojifunza kutokana na mantiki ya mahubiri haya – hizo heri ndizo mahubiri yenyewe. Sehemu inayobaki ya mafundisho Yake ni jinsi ya kufanyia kazi mahubiri hayo – au, jinsi ya kuwa na hizo hali za moyo.

Baadaye katika mafundisho hayo, Yesu atafundisha kwamba hali za moyo zilizo nzuri ndiyo tofauti kati ya maisha yaliyojaa nuru (usafi, kweli na furaha), na maisha yaliyojaa giza, au yasiyokuwa na furaha (Mathayo 6:22, 23). Anaongezea maelezo kwamba, wakati maisha yetu yanapojaa giza kwa sababu ya kuwa na hali mbaya moyoni, yanaweza kuwa na giza kweli kweli, na hali yetu ya kutokuwa na furaha inaweza kuwa kubwa sana.

Tunaweza pia kuongezea hapa kwamba, watu kama Adolf Hitler, au Joseph Stalin, au viongozi wengine waovu wanatekeleza mauaji ya halaika kwa sababu wana hali ya moyo isiyokuwa nzuri, inayoweza kuleta giza kubwa sana katika maisha ya mamilioni ya watu. Ndiyo sababu Yesu alihubiri na kufanyia kazi kitu tunachoweza kukiita "Kujikagua Kutoka Shingoni Kwenda Juu" katika faragha Yake ya kwanza.

Hali Za Moyo Zinazofanya Mtu Aje

Zile hali nane za moyo zinagawanyika katika mafungu mawili yenye hali nne. Kuna mtindo unaojitokeza katika Maandiko wakati Mungu anapochagua viongozi kwa ajili ya kazi Yake. Hao viongozi wanakuwa na kitu tunachoweza kukiita "mambo yanayowafanya waje", kisha, "mambo yanayowafanya waende". Wanamjia Mungu kwa njia yenye maana sana, kabla ya kupata nafasi ya kwenda kwa ajili ya Mungu na kuzaa matunda. Zile hali nne za kwanza za moyo zinawakilisha hali zinazohusika katika kumjia Mungu, na zile za pili zinaonyesha hali zinazohusika na kwenda kwa ajili ya Mungu.

Mambo mengine kama vipawa yanaweza kukuzwa katika upweke, lakini tabia lazima izalishwe katika kuchanganyikana na watu, au, wakati tunapokuwa katika mahusiano na watu. Zile hali nne za kwanza za moyo zinazaliwa pale mlimani, au katika kile ambacho baadaye Yesu anakiita "chumba chetu cha ndani" au, katika sisi kumjua Mungu kibinafsi (Mathayo 6:6). Tunajifunza na kukuza zile hali nne za kwanza za moyo katika mahusiano yetu binafsi na Mungu, lakini zile zingine zinazofuata lazima zikuzwe na kujulikana wakati tunapokuwa katika mahusiano na watu.

Maskini Katika Roho

Hali ya kwanza ya moyo ni hii: "Wamebarikiwa walio maskini katika roho kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao" (Mathayo 5:3, TLR). Hii hali ya kwanza ya kubarikiwa inahusiana na lile swali ambalo viongozi wa dini walimwuliza Yohana Mbatizaji,

kwamba, “Unasemaje juu yako mwenyewe?” (Yohana 1:22, TLR). Bila ya kuwa na hali nzuri juu yetu wenyewe hatutaweza kuwa mojawapo ya majibu ya Bwana wetu.

Ahadi yenye kueleza baraka iletwayo na hali hiyo ya moyo katika maisha ya mwanafunzi maana yake ni kwamba sisi wenyewe binafsi tunakuwa tumemfanya Yesu Kristo kuwa Mwokozi wetu, Bwana na Mfalme. Kuwa sehemu ya ufalme wa mbinguni maana yake nyingine ni kusema sisi ni wananchi wa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana – Yeye ambaye ndiye Jibu. Hiyo ndiyo hali ya kwanza ya moyo tunayopaswa kuwa nayo kama tunataka kuwa sehemu ya Ufumbuzi au majibu kwa mahitaji ya binadamu, ambao Kristo anataka kuleta kwa watu wanaoumia na kuteseka katika dunia hii, kupitia wanafunzi Wake.

Wataalamu wa Biblia wanatuambia kwamba maneno “maskini katika roho” yanaweza pia kumaanisha “waliovunjika rohoni”. Maana yake ni kwamba hali hii inaeleza hali ya kuvunjika – ambayo ni kitu tunachokiona katika maisha ya wale ambao Mungu anawaita na kuwawezesha kwa ajili ya huduma maalum. Unaposoma Biblia, ona jinsi Mungu anavyofundisha hii hali ya kwanza ya moyo kwa wale anaowaita kufanya kazi kubwa kwa ajili ya utukufu Wake. Kwa mfano: Yakobo alipitia hali hii ya kuvunjwa alipomenyana usiku kucha na malaika (ktk Mwanzo 32:24-32).

Watu kama Yakobo, Musa na mtume Petro walipaswa kujifunza masomo matatu wakati Mungu alipokuwa anawafanya maskini katika roho: Walijifunza kwamba wao si kitu; wakajifunza kwamba ni kitu, halafu wakajifunza kile ambacho Mungu anaweza kufanya na mtu ambaye amejifunza kwamba yeye si kitu. Hii hali ya moyo ya kwanza aliyofundisha Yesu, inaposemwa kwa namna nyingine ambayo watu wanaipenda sana, inakuwa hivi: “Umebarikiwa unapofikia mwisho wako. Wewe unapopungua, Mungu anazidi ndani yako, na utawala Wake” (5:3).

Yaani kwa neno moja tu, hali ya neema ambayo Yesu aliitaja kuwa ni maskini katika roho, ni unyenyekevu. Unyenyekevu ni dhana ngumu sana kuielewa. Ukifikiri wewe ni mnyenyekevu, ukweli ni kwamba, sio. Kanisa moja lilimpa mchungaji wao nishani

kwa ajili ya unyenyekevu, lakini wakamnyang'anya kwa sababu kila Jumapili alikuwa anaivaa! Tunaonyesha tumefahamu unyenyekevu wakati tunapoomba hivi: "Ee Mungu! Mimi si jibu. Siwezi hata kutatua matatizo yangu binafsi, na siwezi kutatua ya watu wengine. Lakini, ninajua kwamba Wewe waweza! Wewe waweza kuwa Ufumbuzi wao. Ukiwa ndani yangu, nami niwe na mahusiano na Wewe, basi nina uwezo wa kuwa chombo na njia ya kupitisha Ufumbuzi Wako na jibu Lako, ninapohusiana na watu na matatizo yao."

Wenye Kuomboleza

Hali ya pili ya moyo ni hii: "Wamebarikiwa wale wenye kuomboleza, kwa sababu watafarijiwa" (5:4, TLR). Yesu anatupa somo kuhusu mambo tunayothamini. Je, tunajihesabu kuwa tumebarikiwa wakati tunapo-omboleza? Yesu hapa anatuahidi baraka maalum na faraja katika nyakati zetu za maombolezo. Ukweli anaokazia hapa ni kwamba, wale wenye kuomboleza wamebarikiwa!

Sulemani, aliyekuwa mwanadamu mwenye hekima kuliko wote waliowahi kuishi, anakubaliana na Yesu anapoandika hivi: "Ni afadhali kwenda kwenye nyumba ya maombolezo kuliko kwenye nyumba yenye karamu, maana, huo ndiyo mwisho wa watu wote, na walio hai watatilia maanani. Huzuni ni bora kuliko kicheko, kwa sababu, sura ya huzuni hufanya moyo kuwa bora. Moyo wa mwenye hekima uko katika nyumba ya maombolezo, lakini moyo wa wapumbavu uko katika nyumba ya furaha. … "Siku ya mafanikio, furahi, lakini siku ya matatizo, fikiri: Hakika Mungu amepanga moja kama alivyopanga ile nyingine pia" (ktk Mhubiri 7:2-4, 14, TLR).

Yaani, "Wamebarikiwa wale wenye kuomboleza." Sulemani anaandika kwamba ni tukio la kugusa sana tunapokwenda kwenye msiba na kuona mwili wa yule tumpendaye au kumjua aliyeondoka maishani hapa. Tunaguswa sana kwa sababu tunajua kwamba si swala la kama, bali ni lini na sisi tutakuwa katika hali kama hiyo. Sulemani anatangaza hapa kwamba mambo tunayothamini yanalingana zaidi na mambo tunayothamini milele ambayo Mungu

anataka kutufundisha tunapokuwa kwenye msiba. Basi, ni afadhali kwenda msibani kuliko kwenda kwenye karamu au sherehe.

Wakati mwingine waamini wanakuwa na mawazo ya makosa kwamba, kama wataonyesha hali ya kuomboleza kwa ajili ya mpendwa wao aliyeondoka, imani yao ni dhaifu. Yesu alihudhuria msiba wa mtu aliyempenda sana, na aliomboleza mpaka wakasema, “Oneni jinsi alivyompenda!” (ktk Yohana 11:35, 36, TLR). Maana nyingine ya msingi ya baraka hii ya pili ni kwamba, tusifiche wala kuzuia huzuni yetu.

Paulo aliandika kwamba, tunapowapoteza hawa tunaowapenda walio waamini, hatupaswi kuomboleza kama wasioamini, ambao hawana matumaini ya kumwona tena huyo aliyeondoka (1Wathes. 4:13). Wakati Daudi alipofiwa na mtoto, alionyesha matumaini na majonzi ya mtu mtauwa aliposema hivi: “Mimi nitakwenda kwake, lakini yeye hatarudi kwangu” (ktk 2Samweli 12:23, TLR). Matumaini yetu ni kwamba tutamwona huyo mpendwa mbinguni, ambaye naye alikuwa anamjua Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi. Lakini, kuomboleza kwetu kwa halali kabisa kumejengwa kwenye ukweli usiokanika kwamba, tutaishi maisha yetu yaliyobaki hapa duniani bila yeye.

Tukitaka kugundua baraka na faraja ambayo Yesu aliahidi katika kipindi chetu cha kuomboleza, lazima tumruhusu Mungu atumie kuomboleza kwetu kutusogeza katika njia tatu: Kwanza kabisa: Tunapaswa kuruhusu maombolezo yetu yatufikishe mahali pa kuuliza maswali sahihi – hata kama ndiyo kwa mara ya kwanza katika maisha yetu. Watu wengi hupitia katika maisha bila ya kuuliza maswali sahihi. Lakini, kuna maswali mengi ambayo Mungu anataka kutuuliza wakati tunapokuwa katika kuomboleza.

Ayubu ni mfano mzuri wa hili. Alifiwa na watoto kumi, akapoteza kila kitu alichokuwa nacho, halafu afya yake ikatoweka. Katika muda wote wa mateso na hasara kubwa, aliruhusu maombolezo yake kumfikisha mahali pa kuuliza maswali sahihi. Aliuliza maswali ya maana. Kwa mfano: “Mtu hufa. Analala chali. Roho inamtoka. Anakwisha – baada ya hapo, yuko wapi? Je, mtu

akifa, ataishi tena?" (ktk Ayubu 14:10-14, TLR). Huo ni mfano kuhusu maswali sahihi ambayo Mungu anataka tuulize.

Njia ya pili ambayo Mungu anataka kutusogeza tunapokuwa katika maombolezo ni kwamba, angependa maombolezo yetu yatufikishe mahali tutakaposikia majibu Yake kwa maswali yetu sahihi. Ayubu alipata jibu kubwa sana kwa swali lake, wakati alipokuwa katikati ya mateso yake makubwa. Alipokea mafunuo kuhusu Masiya. Alipaza sauti na kusema hivi: "Najua Mkombozi wangu anaishi, na kwamba mwishoni atasimama juu ya dunia" (ktk Ayubu 19:25, TLR).

Yawezekana Mungu asitupe mafunuo makubwa kama alivyofanya kwa Ayubu, lakini Biblia imejaa majibu Yake kwa maswali hayo sahihi. Mfano mzuri ni Zaburi ya Kichungaji ya 23, yenye majibu mengi sana.

Yesu alitupa jibu zuri sana alipohudhuria ule msiba, mahali alipolia sana. Pale kaburini alimpa changamoto mpendwa mmoja ambaye naye alikuwa analia, kwa maneno haya: "Mimi ndiye ufufuo na uzima. Aniaminiye Mimi, hata akifa, ataishi. Na yeyote anayeishi na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Je, unaamini hayo?" (Yohana 11:25, 26, TLR).

Swali la Yesu baada ya hiyo changamoto nzito inatufikisha kwenye njia ya tatu ambayo Mungu anataka kuitumia kutusogeza kuelekea baraka ile iliyoahidiwa na Yesu wakati tunapo-omboleza: Tukitaka kugundua baraka na faraja ambayo Yesu aliwaahidi wenye kuomboleza, tunapaswa kuruhusu maombolezo yetu kutufikisha mahali ambapo tunaamini na kutegemea majibu ya Mungu kwa maswali yetu sahihi.

Tunapoamini majibu ya Mungu kwa maswali yetu sahihi, tutagundua kwamba baraka na faraja alizoahidi Yesu kwa wanao-omboleza ni kitu kinachoitwa "wokovu" katika Biblia. Hilo neno maana yake ni "ukombozi". Tunaweza kujua ukombozi wa kwanza wa wokovu au ukombozi tunaohitaji kutoka katika huzuni na kugandamizwa na maisha. Tunaweza kupitia hali za muhimu sana maishani mwetu wakati maombolezo yetu yanapotufanya tuulize, tusikilize na kuamini.

Mantiki ya mafundisho haya inafunua tafsiri na maana nyingine katika maisha yetu, ya hiyo hali ya pili ya moyo. Mkakati wa Yesu kwenye hii faragha ni huu: “Tazameni chini ya mlima. Je, mnawaona hao watu wote huko chini? Hao wote wanaumia. Hivi mnafikiri kweli kwamba mnaweza kushuka huko chini na kuwa sehemu ya ufumbuzi wa matatizo yao na sehemu ya majibu wanayohitaji kupata katika matatizo yao mazito bila ya ninyi kuumia wenyewe?” Neno “huruma” maana yake “kujisikia pamoja na”. Unawezaje kujisikia wanavyojisikia watu walioumia, kama wewe mwenyewe huumii?

Mtu mmoja amesema hivi: “Mwinjilisti ni maskini mmoja akimweleza maskini mwingine mahali penye mkate”. Mponyaji aliyeumia, ambaye ameumia na kufarijiwa na Mungu, ni “Moyo mmoja ulioumia, ukiambia moyo mwingine ulioumia, mahali Mfariji alipo, na kwamba ni Nani”. Watu wengi watakwambia kwamba walimwamini Mungu na kujua habari za Mungu, lakini hawakumjua Mungu mpaka walipofikia kiwango cha mateso ambacho Mungu tu aliweza kutoa faraja. Waliposukumwa kumgundua Mfariji, walijenga uhusiano na Mungu.

Hali hii ya moyo inaelezwa kwa maneno mengine rahisi tu yanayopendwa sana, hivi: “Umebarikiwa unapojisikia kwamba umepoteza unachokipenda sana. Hapo ndipo itakapowezekana wewe kukumbatiwa na Mmoja (aliye) mpendwa sana kwako” (Mathayo 5:4 – Tafsiri Ya Ujumbe).

Tunagundua tena jambo lingine katika hii hali ya pili ya moyo tunapoiunganisha na ile ya kwanza. Mara nyingi tunaomboleza tunapokuwa katika kujifunza kwamba sisi ni maskini katika roho. Hofu ya kushindwa inawasumbua watu wengi na kuwasukuma sana, kwa sababu inasikitisha mtu anaposhindwa. Tunaomboleza sana tunaposhindwa. Lakini kushindwa kwa mtu binafsi ni chombo kizuri sana ambacho Mungu hutumia kutufanya tutambue kwamba hatuwezi lolote pasipo Yeye. Musa na Petro walikuwa wanaomboleza machungu ya kushindwa vibaya sana walipokuwa wanajifunza kwamba wao ni maskini katika roho, kabla ya Mungu kuweza kuwatumia kwa nguvu na kwa namna kubwa sana.

Wapole

Hali nyingine ya moyo ambayo Yesu analeta mbele yetu inahusu mambo tunayotaka. “Wamebarikiwa walio wapole, kwa sababu watairithi dunia.” Hivi upole ni nini? Pengine upole ndicho kitu kisichoeleweka vizuri, na kinachotumiwa vibaya katika hizi hali zote nane za moyo katika mahubiri haya. Upole si udhaifu. Tunamsikia Yesu Mwenyewe akisema, “Mimi ni mpole” (ktk Mathayo 11:29, TLR). Unapofikia mahali pa kumjua Yesu Kristo wa Maandiko, utatambua kwamba hakuwa mpole katika maana ya kwamba ni mtu dhaifu au mnyonge.

Agano la Kale linasema kwamba Musa alikuwa mpole kuliko wanadamu wote waliowahi kuishi (ktk Hesabu 12:3). Unaposoma Agano la Kale na kumjua Musa vizuri zaidi, utagundua kwamba yeye hakuwa mtu dhaifu. Yesu hakuwa dhaifu, wala Musa pia, kutokana na upole wao!

Labda tutaona maana ya “upole” katika Biblia, tukifikiri kuhusu farasi mwenye nguvu, ambaye hajafundishwa. Ni mnyama mwenye nguvu sana, na mwenye nia yenye nguvu. Watu wenye utaalamu katika hili wanaweka lijamu juu ya kichwa cha farasi huyo polepole sana, na kwa uangalifu sana wanahakikisha imefika mpaka katika mdomo wake. Kisha wanamfungia kiti cha kukalia kwenye mgongo wake. Wakisha fikia mahali pa huyo farasi kukubali ile lijamu pamoja na utawala wake, na mtu kuketi kwenye kiti mgongoni mwake – yaani, nia ya yule farasi inapokuwa imevunjwa – amekubali utawala na mamlaka – huyo farasi bado ni mwenye nguvu sana, lakini sasa amekuwa mpole.

Sauli wa Tarso alipokutana na Kristo mfufuka akiwa njiani kwenda Dameski, yafuatayo yanaweza kuwa maneno Bwana aliyomwuliza Sauli – kwa njia nyingine. “Kwa nini unanitesa? Kwa nini unashindana na lijamu? Wewe ndiye unayeumia” (ktk Matendo 9:4, 5, TLR).

Lakini, Sauli wa Tarso alipouliza swali hili: “Bwana, unataka mimi nifanye nini?”, hapo alikuwa amekubali utawala wa ile lijamu, ambayo pamoja na mambo mengine, ilikuwa mapenzi ya Kristo

mfufuka kwa ajili ya maisha yake. Hapo ndipo Sauli akawa mpole, na huo ndiyo upole halisi basi.

Yesu alitoa tamko kwamba, “Mimi ni mpole” alipokuwa anatoa mwaliko mkuu sana, kwamba, “Njooni kwangu, ninyi nyote mliochoka na wenye mizigo, nami nitawapa pumziko. Jitwikeni nira Yangu na kujifunza kutoka Kwangu, kwa sababu Mimi ni mpole na mnyenyekevu moyoni, nanyi mtapata pumziko kwa ajili ya nafsi zenu. Maana, nira Yangu ni rahisi na mzigo Wangu si mzito” (ktk Mathayo 11:28-30, TLR).

Katika lugha ya asili iliyotumika kuandika maneno hayo, tunaona kwamba maneno hayo yalisemwa kwa watu waliokuwa wanafanya kazi sana mpaka kuchoka, wakijaribu kubeba mizigo yao mizito kabisa.

Katika mwaliko Wake, Yesu anawaita watu wenye mizigo mizito kuja na kujifunza kuhusu mzigo Wake, moyo Wake na nira Yake. Yeye anataka wajifunze kwamba mzigo Wake si mzito. (Hii ni ajabu kwa sababu Yeye alikuwa amebeba dunia nzima mabegani Mwake.) Anataka wajifunze kwamba moyo Wake ni mnyenyekevu na mpole, na anataka kuwafundisha kwamba nira Yake ndiyo inafanya mzigo Wake kuwa mwepesi, na maisha Yake kuwa rahisi.

Nira si mzigo. Nira ni chombo kinachowezesha mnyama kama fahali (ng’ombe dume) kusogeza mzigo mzito. Bila shaka wengi wetu tumewahi kuona magari yanayovutwa na ng’ombe yaliyojaa vitu mpaka juu. Kinachowezesha mnyama huyo mwenye nguvu sana kutawaliwa mpaka aweze kuhamisha au kusogeza mizigo hiyo mizito sana, ni nira.

Huu mfano rahisi tu lakini wenye maana sana, unaeleza maana ya upole. Hali hii ya moyo ya tatu ambayo ni upole, maana yake ni nguvu zilizotawaliwa. Kimsingi, anachofundisha Yesu ni hiki: “Mimi huvaa nira ya mapenzi ya Baba Yangu kila siku.” Kumbuka alisema hivi: “Siku zote Mimi hufanya mambo yanayompendeza Baba” (ktk Yohana 8:29, TLR). Hiyo ndiyo nira aliyovaa Yesu. Alikubali nira ya Baba, na alikuwa anatawaliwa na Baba Yake mia kwa mia, wakati wote. Hiyo ndiyo hali ya moyo ambayo Yesu anawafundisha wanafunzi Wake – upole.

Nira iliyokuwa inashika vizuri, na iliyokuwa imesuguliwa na seremala mzuri, ilifanya maisha ya mnyama husika kuwa rahisi; na mzigo wake kuwa mwepesi. Seremala kama Yesu angetengeneza nira ambazo zilikuwa zinakaa vizuri, ambazo zilikuwa laini ndani ili mnyama asikwaruzwe au kuumia. Yesu anafundisha hali ya moyo ya upole kwa sababu anajua kwamba nira anayovaa Yeye kila siku itafanya mizigo kuwa myepesi na mizigo kuwa rahisi kwa ajili ya wale wanaohangaika kutokana na kutokuwa na nira.

Anapofundisha hali ya moyo ya tatu, Yesu ni kama anayesema hivi: “Kuna njia inayofaa ya kuishi maisha yako. Kama utaishi maisha kama Mimi, utagundua kwamba hutalemewa, hutachoka, wala hutafanya kazi kufikia mahali pa kuzidiwa ili kutawala matatizo yako.” Alichokuwa anasema hasa ni hiki: “Shughulika na maisha kama Mimi ninavyofanya. Ukikubali nira Yangu ya upole, utagundua kwamba inaweza kufanya mzigo wako ukawa mwepesi na kufanya maisha yako kuwa rahisi, hata kama unakabiliwa na changamoto kubwa kiasi gani.”

Kwa muhtasari, Yeye anachowafundisha wale watu pale Mlimani ni hiki: “Watu kule chini wanateseka kwa sababu hawajui jinsi ya kuvuta mzigo wa maisha. Wao hawana uwezo wa kusogeza mizigo yao kwa sababu hawana nira. Lakini kama ninyi mtakubaliana na mambo ninayothamini Mimi, na kuishi maisha yenu kwa hali za moyo ninazowapa Mimi, na kufundishwa kwa nidhamu za kiroho ambazo nitawaonyesha wakati mnanifuata Mimi, mtajifunza kitu kuhusu mzigo Wangu, moyo Wangu na nira Yangu, kitakacholeta pumziko katika nafsi zenu.”

Upole ni nidhamu ya matakwa yetu, au ya nia zetu. Maneno “mwanafunzi” na “nidhamu” yanatokana na msingi mmoja katika lugha ya asili. Ahadi ya Yesu inayoambatana na hali hiyo ya moyo yenye baraka ni kwamba, mwanafunzi mpole atairithi dunia. Hii ina maana mbili, kwa urahisi tu: (1) Tunapaswa kutazamia kwamba mwanafunzi wa Yesu atakuwa mtu mwenye nidhamu, na (2) mwanafunzi wa Yesu mwenye nidhamu anapata kila kitu, anapokuwa amevaa Nira ya Yesu na Baba yake maishani mwake mchana kutwa, siku zote.

Wenye Kuwa Na Njaa Na Kiu Kwa Ajili Ya Haki

Hali ya nne ya moyo ni hii: “Wamebarikiwa wale wenye kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki maana, watajazwa” (Mathayo 5:6, TLR). Tunapokuwa wapole, au tunapoweza kusema kwamba Yesu ni Bwana wetu na kwamba tunatoa maisha yetu yatawaliwe Naye, Yesu anafundisha kwamba sasa tunapaswa kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki.

Hapo sasa tunaona utaratibu ukijitokeza, kwamba, hizo baraka zinakuja mbili-mbili. Tunaomboleza tunapokuwa tukijifunza kuwa maskini katika roho, na wakati tunapokuwa wapole, tutakuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki. Haki ni hali ya kuwa sahihi, au kufanya kilicho sahihi. Kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki ni kuwa na njaa na kiu ya kujua kilicho sawa – hasa kujua kilicho sawa kwa ajili yako wewe.

Mara tu Paulo alipokuwa mpole pale njiani kuelekea Dameski, alitaka kujua kilicho sahihi kwake. Alipomwita Yesu “Bwana” na kuuliza Bwana wake anataka afanye nini, hakuwa anaonyesha upole tu. Alikuwa pia anaonyesha nini maana ya kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki.

Maelezo kuhusu hasira ya haki, au ile ya Yesu tunayosoma habari zake katika Injili ni kwamba kile ambacho viongozi wa kidini walikuwa wanakifanya katika Hekalu la Mungu kilikuwa kinyume na kilichokuwa sawa. Ona ari ya Yesu kufanya mapenzi ya Baba Yake. Halafu tambua kwamba shauku ya kutaka kutenda kilicho sawa ni pamoja na shauku ya kupambana na kurekebisha kisichokuwa sawa.

Katika haya Mahubiri ya Mlimani, ona mkazo wa Yesu kwenye umuhimu mkubwa sana wa haki: Hali ya moyo inayotajwa mwisho ni hii: “Wamebarikiwa wale wanaoteswa kwa ajili ya haki, kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao” (ktk Mathayo 5:10, TLR). Hali mbili za moyo kati ya zile nane, zinahusiana na haki. Baadaye katika sura hii, Yesu anafundisha hivi: “Kwa sababu, nawaambia hivi: haki yenu isipozidi ile ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni” (5:20, TLR). Vile vile mwanzoni mwa sura ya sita anafundisha hivi: “Mwe waangalifu.

Msifanye matendo yenu ya haki mbele ya watu, ili mwonekane na watu." Katika nusu ya pili ya sura ya sita, anafundisha mambo ya kuthamini. Anafikia mwisho wa mafundisho Yake kuhusu mambo ya kuthamini anapotoa cha kwanza cha kuthamini: "Lakini, utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake …" (6:33, TLR).

Ahadi inayoambatana na hali hii ya moyo ni kwamba, mwanafunzi atajazwa haki anayoionea njaa na kiu. Lugha ya asili ya Kiyunani inatoa wazo kwamba wahusika watajazwa na haki mpaka wakaribie kushindwa kuvuta hewa. Hii pia inamaanisha kwamba watajazwa kikamilifu na Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye ndiye Haki yenyewe, na watajazwa na njaa na kiu ya kutaka kujua anachotaka wao wafanye.

Hapa ona kwamba hali hii ya moyo haisemi, "Wamebarikiwa wanaosikia njaa na kiu kwa ajili ya furaha, kwa sababu watafurahishwa kabisa." Wala siyo "Wamebarikiwa wenye kusikia njaa na kiu kwa ajili ya kutoshelezwa." Wala siyo, "Wamebarikiwa wenye njaa na kiu ya kufanikiwa, maana watafanikiwa sana." Hicho sicho kinachoahidiwa hapa. Hali ya moyo inayotajwa hapa ni hii: "Wamebarikiwa wale wenye kusikia njaa na kiu kwa ajili ya haki." Na ahadi ni kwamba watajazwa na haki na shauku ya kutenda kilicho sawa.

Mashujaa walioshughulikia utovu wa haki – kama wale waliofanikisha kuondolewa kwa utumwa – walikuwa wanafunzi wa Yesu Kristo kwa dhati. Pamoja na kuwa na njaa na kiu ya kilicho sawa, walikuwa pia na shauku ya kushambulia kisichokuwa sawa. Watu waliopokea Zawadi ya Nobel ya Amani kama vile Martin Luther King na Nelson Mandela ni watu walioonyesha njaa na kiu yao kwa ajili ya haki kwa kupiga kelele kwa amani tu dhidi ya ubaguzi wa rangi na utaifa. Ukifuatilia neno "haki" katika Biblia yote, utaona kwamba Yesu alikuwa anakwenda sawa na Maandiko alipokazia sana dhana ile kwamba, mwanafunzi aliyejaa haki atakabiliana vilivyo na kutokuwepo kwa haki.

Andiko moja zuri sana la haki ni hili: "Toa dhabihu ya haki, na uweke matumaini yako katika Bwana" (Zaburi 4:5, TLR). Mwandishi wa Zaburi ameshindwa kulala kwa sababu yeye ni mtu

wa kiroho anayefanya kinachotakiwa badala ya kilicho sawa. Anaamua kwamba atajitoa kwa hali yoyote ile ili kufanya kilicho sawa. Hapo anapata amani na analala kwa starehe kabisa. Shauku yake kwa ajili ya uamuzi huo ni kwamba, anajua kuwa amezungukwa na watu wanaotafuta kitu kizuri. Wanatafuta mtu atakayetenda kilicho sawa badala ya kinachotakiwa.

Yesu anapokazia uaminifu binafsi na haki ya wanafunzi Wake, anatoa tamko kwamba sababu moja ya wale watu waliokuwa chini ya mlima kuwa na hali mbaya na kutokuwa na furaha ni kwamba wanafanya kila kitu kinachofanywa na kila mtu. Wao wanafanya kinachotakiwa badala ya kufanya kilicho sawa.

Andiko lingine ambalo linafaa kutajwa kutoka katika mingi iliyoko inayohusu haki linasema kwamba watu wa Mungu wanapaswa kuitwa “Miti ya haki, pando la Bwana, ili Yeye aweze kutukuzwa” (ktk Isaya 61:3, TLR).

Ni mpango wa Mungu – na ndiyo mkakati wa Yesu katika faragha hii – kuwapata wanafunzi watakaokuwa njia za kupitishia haki, wanaporudi katika lile kundi la watu walioko chini ya mlima, wenye kuwakilisha watu waliopotea katika dunia hii. Mpango Wake ni kwamba wanafunzi Wake wapandwe katika dunia hii kama miti ya haki, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Sura Ya Pili

"Hali Za Moyo Zinazosababisha Kwenda"

(Mathayo 5:7-12)

"Wamebarikiwa wenye huruma, kwa sababu watapokea huruma. Wamebarikiwa walio safi katika moyo, kwa sababu watamwona Mungu. Wamebarikiwa wanaoleta amani, kwa sababu wataitwa watoto wa Mungu. Wamebarikiwa wale wenye kuteswa kwa ajili ya haki, kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao.

"Mmebarikiwa ninyi mtakapotukanwa na kudharauliwa, na watakapowasemea maovu ya kila namna kwa uongo, kwa ajili Yangu. Furahini sana, kwa sababu thawabu yenu ni kubwa sana mbinguni, kwa sababu ndivyo walivyowatesa manabii waliokuwa kabla yenu" (ktk Mathayo 5:7-12, TLR).

Kupanda Mlima

Mtaalamu mmoja maarufu sana anaandika kwamba haya mahubiri ni sawa na kupanda mlima: Hali za kwanza mbili – kuwa maskini katika roho na kuomboleza – hutufikisha nusu ya mlima. Upole unatufikisha robo tatu ya mlima, na kuwa na njaa na kiu pamoja na kujazwa haki hutufikisha juu ya mlima. Yaani, tunaupanda mlima wakati tunapojifunza zile hali zinahusu kuja.

Mwanafunzi anapojifunza hali zinazopelekea kufika juu ya mlima, atakuwa mtu wa namna gani kabla ya kuanza kushuka kwake upande wa pili wa mlima na kujifunza zile hali za kwenda ambazo Kristo anataka ajifunze? Kwa kuwa wamekwisha jazwa na haki, je, ni sawa na Mafarisayo? Je, wanawadharau watu na kuwaambia sura na mistari yenye kuhukumu tabia za wale wanaowajua? Hizo hali zinazosababisha kwenda zitajibu maswali haya.

Wenye Rehema

Hali ya tano ya moyo ni, “Wamebarikiwa wenye rehema, kwa sababu watapata huruma” (ms. 7, TLR). Neno “rehema” maana yake ni “upendo usiokuwa na masharti”. Wakati Daudi anapoandika kwamba huruma ya Mungu itamfuata siku zote za maisha yake, anamaanisha hivyo hivyo. Daudi anaamini kwamba upendo wa Mungu usiokuwa na masharti yoyote utamfuata siku zote za maisha yake (Zaburi 23:6).

Baada ya matisho yote ya Wayahudi kushindwa na WaBabeli kutimia, Yeremia aliandika Maombolezo yake. Alipokuwa anaandika, alipata ufunuo. Kimsingi, Mungu alimfanya ajue hivi: “Mimi siachi kamwe kuwapenda watu Wangu, ewe Yeremia!” Ndipo alipoandika kwamba rehema na rehema za Mungu hufanywa upya kila asubuhi (ktk Maombolezo 3:22, 23, TLR).

Mstari wa kwanza katika unabii wa Malaki ni huu: “Neno la Bwana kwa njia ya Malaki: ‘Nawapenda, asema Bwana’!” Ujumbe mzima wa nabii Hosea ni upendo wa Mungu usio na masharti. Mungu siku zote amekuwa akipenda, Naye ni upendo usiokuwa na masharti (1Yohana 4:16). Rehema za Mungu hutuzuia kupata kile tunachostahili kwa sababu ya dhambi zetu, na neema ya Mungu hutupa sisi aina zote za baraka, tusizostahili kupata. Kwa maneno mengine, hali hii ya moyo inaweza kuelezwa hivi: “Wamebarikiwa watu waliojawa upendo wa Mungu, usio na masharti yoyote”.

Inapendeza sana kujua kwamba neno hili “rehema” linapatikana mara mia tatu sitini na sita katika Biblia, kwa sababu Mungu alijua kwamba tungelihitaji kila siku – na siku moja zaidi katika miaka mirefu. Katika Agano la Kale, rehema za Mungu hutajwa mara mia mbili na themanini. Siku zote Mungu amekuwa Mungu wa upendo usiokuwa na masharti yoyote.

Ahadi ya Yesu kwa wenye rehema ni kwamba, “Watapata huruma”. Hiyo haimaanishi kwamba watapokea rehema kutoka kwa Mungu na kwa wale wanaowaonyesha rehema, bali pia kwamba watakuwa vyombo vya kupitisha upendo wa Mungu usiokuwa na masharti yoyote kwa watu wanaohitaji kupendwa bila masharti yoyote.

Kama tutashuka mlima na kuwa sehemu ya jibu la Kristo kwa wale wenye kuumia, lazima tujazwe na upendo wa Mungu usiokuwa na masharti. Wale wanafunzi ambao ndiyo majibu na ufumbuzi wa Yesu, si Mafarisayo wenye kujihesabia haki, bali ni vyombo vya kupitisha upendo wa Mungu na Kristo, usiokuwa na masharti yoyote. Kujazwa na haki ni kujawa upendo wa Mungu – kwa maneno ya Yesu.

Walio Safi Katika Moyo

Mara nyingi tunapopenda, tunafanya hivyo kwa nia ya ubinafsi. Ndiyo sababu hali ya moyo inayofuata ni hii: "Wamebarikiwa walio safi katika moyo, kwa sababu watamwona Mungu" (ms. 8, TLR). Mfuasi wa Kristo anapopenda, si kwa sababu wana hitaji binafsi wanalojaribu kutosheleza. Wao hupenda kwa sababu wamejaa upendo wa Kristo aliye hai, mfufuka, na makusudi yao ni safi kabisa.

Neno "safi" katika mstari huu ni la Kiyunani ambalo linatafsiriwa mahali pengine kama "kutakasika". Hii inaonekana wakati Yakobo anapotumia neno hilo hilo kwa Kiyunani (ktk Yakobo 4:8). Kiini cha fundisho hili ni kwamba, wakati mwanafunzi anapopenda kwa upendo wa Mungu usiokuwa na masharti, makusudi yoyote ya kibinafsi yatasafishwa na kuondolewa moyoni mwake. Maana katika maisha ni kwamba, tunapaswa kuomba kila siku kwamba, kama kuna kitu kingine katika mioyo yetu isipokuwa upendo wa Kristo, Roho Mtakatifu akiondoe.

Tunapowatendea watu kitu chema, mara moja wanatilia mashaka makusudi yetu. Lakini mwanafunzi wa Yesu mwenye huruma anaweza kuwaambia wale anaowapenda, hivi: "Sitaki chochote kutoka kwenu isipokuwa nafasi ya kuwapenda kwa upendo wa Kristo."

Ahadi ya Yesu kwa walio safi katika mioyo ni kwamba watamwona Mungu. Vyombo vya kupitisha upendo wa Kristo kwa makusudi safi kabisa humwona Mungu wanapopitisha upendo wote wa Kristo unaotumika katika maumivu yote ya watu wote wanaoteseka katika dunia hii. Upendo wa Mungu unapopitia kwao,

wanaishi katika Mungu na Mungu ndani yao, kulingana na maneno ya Mtume wa Upendo (ktk 1Yohana 4:16).

Waleta Amani

Hali ya saba ya moyo ni hii: "Wamebarikiwa wanaoleta amani, kwa sababu wataitwa watoto wa Mungu". Kiini cha hali hiyo ya moyo ni kwamba mwanafunzi aliye jibu na ufumbuzi wa Yesu ni mtumishi anayeleta upatanisho. Mojawapo ya vyanzo vya matatizo ya kutisha sana huko chini ya mlima ni ile hali ya kutenganisha. Watu wametengana na Mungu, wametengana na wengine, na hata na wao wenyewe. Yesu anawahimiza wanafunzi Wake kujifunza na kupata hali za moyo zenye nguvu, zitakazowafanya wao kujua upatanisho katika maeneo hayo matatu na kisha wawe watumishi wa upatanisho watakaporudi kwenye makundi ya watu huko chini ya mlima.

Paulo anaandika kwamba kila aaminiye aliyekutana na muujiza wa upatanisho na Mungu kwa njia ya Kristo, ameagizwa na kutumwa na ujumbe na huduma ya upatanisho (ktk 2Wakor. 5:14 hadi 6:2). Kutokana na fungu hilo, mwanatheolojia mmoja ameandika hivi: "Ni mapenzi ya Mpatanishaji kwamba waliopatanishwa wawe mawakala wa upatanisho katika maisha ya wale ambao bado hawajapatanishwa." Kimsingi, huo ndiyo mkakati wa Yesu anapofundisha hali ya moyo ya saba mahali hapa.

Katika kipindi cha Vita Baridi, tabibu mmoja katika mojawapo ya kambi mbaya sana za kazi za kitumwa huko Siberia – Urusi – aliokoka. Baada ya kumwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wake, huyu tabibu Myahudi aliyeitwa Boris Kornfeld aliamua kwamba atakuwa mtumishi wa upatanisho katika mahali hapo pa kutisha. Akamfanyia upasuaji mgonjwa mmoja, na baada ya upasuaji huo, akamwambia habari za Yesu Kristo. Kwa tendo lake hilo la kijasiri, aliuawa usiku huo akiwa amelala. Mgonjwa aliyemtibu alipona, na hatimaye akashuhudia duniani kote habari za ubaya wa hizo kambi za utumwa. Jina la huyo mgonjwa aliyepona ni Alexander Solzhenitsyn.

Huyo tabibu na mwanafunzi wa Yesu hakujua kwamba mgonjwa wake angekuja kuwa mtu maarufu na kuandika vitabu vingi vizuri. Yeye alifanya tu kile ambacho Yesu alifundisha wakati akitoa maelezo kuhusu hali ya saba ya moyo. Ahadi ya Yesu kwa watumishi hawa wa upatanisho ni kwamba wataitwa watoto wa Mungu. Mungu alikuwa na Mwana mmoja tu, naye akawa mishenari – aliyetumwa. Si ajabu basi kwamba Mungu atawahesabu wale waliotumwa kama watoto Wake. Tena, hakuna jinsia hapa – wote – waume kwa wake – ni watoto wa Mungu – wana wa Mungu.

Wanaoteswa

"Wamebarikiwa wale wenye kuteswa kwa ajili ya haki, kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao". Hali hii ya saba imeunganishwa na ile ya nane.

Boris Kornfield alitoa maisha yake ili kuwa wakala wa upatanisho kwa ajili ya Alexander Solzynitzen. Hayo ndiyo yamekuwa maisha ya watumishi wa upatanisho katika historia ya kanisa. Ndiyo sababu hali ya moyo ya saba ni hii: "Wamebarikiwa walio mawakala wa upatanisho" na ya nane ni: "Wamebarikiwa wale wenye kuteswa kwa ajili ya haki, kwa sababu ufalme wa mbinguni ni wao". Wale wanaoteswa kwa sababu ni watumishi wa upatanisho kweli wanakiri utawala wa Mfalme katika maisha yao, hata kama itawagharimu uhai wao.

Hebu ona kwamba haisemi tu "Wamebarikiwa wenye kuteswa" kwa sababu yoyote ile – hasa kwa sababu ya mambo wanayojiletea wenyewe. Ni "wamebarikiwa wale wanaoteswa kwa ajili ya haki". Kwa sababu wamewaambia wengine Injili – kwa sababu wamejitambulisha na Yesu Kristo – watateswa. Bila shaka unaona ni kwa nini hizo hali mbili za mwisho zinaunganika.

Watumishi wa upatanisho huteswa kwa sababu wao huwekwa katikati ya magomvi na matengano. Wao huenda mahali ambapo watu waliotengana hupigana. Hebu fikiri maeneo yenye vurugu duniani – kama vile Mashariki ya Kati au pengine popote penye vurugu. Watumishi wa upatanisho huenda huko, nako ni mahali pa hatari sana.

Yesu anafundisha hizi hali nane nzuri sana, kisha, kuanzia mstari wa kumi na moja, anaanza kutoa maana yake katika maisha. Ona kwamba mara nane anatumia maneno ya jumla – Wamebarikiwa hao – wamebarikiwa wale. Halengi mtu yeyote hapo. Lakini, kuanzia mstari wa kumi na moja, anasema hivi: “Mmebarikiwa ninyi mtakapotukanwa na kudharauliwa, na watakapowasemea maovu ya kila namna kwa uongo, kwa ajili Yangu”.

Sasa anawageukia wale waliokaa wakimzunguka, na anafanya ujumbe kuwa wa mtu binafsi sasa. Analeta utabiri wa mateso kwa wahusika. Maana ya hali hizo nane za moyo katika maisha inaanza hapa, na mafundisho yatokanayo na hali hizo yataanza kufanyiwa kazi katika maisha kuanzia hapa na kuendelea.

Tungedhani kwamba kama kuna watu wenye hali hizo za moyo nzuri sana katika dunia yetu leo wangepongezwa sana. Lakini, hizi hali za moyo ambazo ni za mwisho zinatueleza kwamba, pamoja na hali hizo nzuri sana za moyoni, mwanafunzi wa Yesu Kristo atateswa. Kwa nini?

Jibu la swali hilo ni kwamba, mwanafunzi mwenye hali hizo za moyo anawakabili watu kwa kuonyesha mfano wa jinsi wanavyotakiwa kuwa. Watu wa dunia hii wanapokabiliwa na maisha ya mwanafunzi mwenye hali hizo za moyo, wana uamuzi wa aina mbili: Wanaweza kukubaliana na mfano huo wa jinsi ya kuishi, na wanaweza kutamani hizo hali za moyo zinazowafanya wawe kama walivyo. Au, wanaweza kumshambulia mwanafunzi anayeonyesha mfano wa mwelekeo na mambo anayothamini Yesu Kristo. Kwa miaka zaidi ya elfu mbili, ulimwengu wa wasiomcha Mungu umekuwa ukiamua hilo la pili.

Muhtasari Wa Hizo Hali Nane

Hizi hali nane za moyo ndiyo mahubiri yenyewe, na mengine yote yanayofuata ni maelezo ya Yesu ya maana katika maisha, ya mahubiri hayo. Mantiki ya mahubiri haya hutupa maelezo ya Mathayo kuhusu yanayohusika kwa mtu anapokuwa Mkristo. Kulingana na Mathayo – kuwa Mkristo si swala la kile ambacho Yesu atakutendea. Mkazo ni: “Utafanya nini kwa ajili ya Yesu? Je,

wewe ni sehemu ya tatizo au ni sehemu ya jibu la Yesu? Je, wewe ni mojawapo ya majibu Yake, au na wewe ni swali lingine tena?"

Hali hizo zilizobarikiwa ni mfano wa tabia zinazohusika kwa Mkristo. Mifano ile minne – chumvi, nuru, mji na mshumaa – inayofuata mara tu baada ya hizo hali, huleta changamoto inayokuja wakati tabia ya Kikristo inapogusa tamaduni za kawaida.

Ni kana kwamba kuna "ikweta ya kiroho" kati ya hali ya nne ya moyo na hali ya tano. Hizi hali nane za moyo zinagawanyika katika sehemu mbili zenye hali nne kila moja. Zile nne za kwanza ni hali zinazohusika wakati mtu anapomjia Kristo, na zile hali nne za pili zinaonyesha hali zinazohusika katika kwenda – au kutoka – kwa ajili ya Kristo. Zile hali nne za kwanza zinajengwa mlimani, pale kileleni, au, katika mahusiano yetu binafsi na Mungu na Kristo. Lakini, zile hali nne za pili lazima tujifunze na kuziendeleza katika mahusiano yetu na watu.

Zile hali za moyo pia zinagawanyika katika makundi manne yenye mambo mawili-mawili, hivi: maskini katika roho anayeomboleza; mpole mwenye njaa na kiu kwa ajili ya haki; mwenye rehema aliye na moyo safi, na waleta amani wanaoteswa.

Kila hali ya moyo yenye sehemu mbili huonyesha siri ya kiroho ambayo lazima kila mwanafunzi wa Yesu aijue kabla ya kuwa sehemu ya ufumbuzi Wake, na kuwa mmoja kati ya majibu Yake. Zile mbili za kwanza – kuwa maskini katika roho na kuomboleza – huonyesha picha hii: "Si swala la ninachoweza kufanya mimi. Ni swala la anachoweza kufanya Yeye."

Zile mbili zinazofuata – upole na kuwa na njaa na kiu kwa ajili ya haki – huonyesha siri hii ya kiroho: "Si ninachotaka mimi, bali anachotaka Yeye." Za tatu – mwenye rehema aliye na moyo safi – huwakilisha siri hii ya kiroho: "Si swala la mimi ni nani au nini, bali Yeye ni nani na nini".

Zile za nne – waleta amani wanaoteswa – huonyesha siri ya kiroho, ambayo lazima tuikiri wakati Kristo anapotutumia, kwamba, "Si chochote nilichofanya mimi, bali alichofanya Yeye." Mtume Paulo anawaandikia Wakorinto kwamba alipofanya huduma yake ya

nguvu katika mji wao, hakuna chochote kilichotoka kwake – kila kitu kilitoka kwa Mungu (ktk 2Wakor. 3:5).

Neno "wamebarikiwa" linapaswa kufafanuliwa. Katika tafsiri zingine linatumika neno "wana furaha". Hii ni sawa na ile furaha ambayo ni tunda la Roho (ktk Wagalatia 5:22, 23). Hii furaha iliyobarikiwa inaweza kuelezwa kwamba ni ile isiyoeleweka vizuri – isiyoleta maana timamu – kwa sababu inatoka kwa Roho Mtakatifu aliyeko maishani mwetu, tena, haitawaliwi na mazingira.

Neno hilo "wamebarikiwa" limetafsiriwa pia kuwa "wamefanikiwa kiroho". Kufanikiwa kiroho hakumaanishi utajiri kiuchumi. Kama mafanikio kiuchumi ndiyo maana ya kubarikiwa, basi hakuna mtume hata mmoja aliyekuwa amebarikiwa. Kwa sababu waliishi kulingana na mafundisho hayo yaliyotolewa na Yesu, hawakuwa matajiri walipokufa vifo vya kutisha sana.

Sura Ya Tatu

"Kobe Kwenye Nguzo"

(Mathayo 5:13-16)

Yesu alifuatisha picha Yake ya tabia kama za Kristo kwa kutoa mifano minne yenye kutuonyesha sisi kinachotokea wakati tabia alizoonyesha kwa hali za moyo tunazopaswa kuwa nazo, zinapokutana na tamaduni za kipagani. Alifundisha hivi: "Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini, chumvi ikipoteza ladha yake, itawekwaje ladha tena? Haiwi na faida tena bali kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya dunia. Mji uliowekwa juu ya mlima hauwezi kufichwa. Wala hawawashi taa na kuiweka chini ya kikapu, bali juu ya kinara cha taa, nayo inatoa nuru kwa wote walio katika nyumba. Basi, acheni nuru yenu ing'ae mbele za watu, ili wapate kuyaona

matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu wa mbinguni" (Mathayo 5:13-16, TLR).

Chumvi Ya Dunia

Yesu anaanza sehemu ya maana ya mahubiri katika maisha yetu, kwa mifano hiyo minne. Mfano wa kwanza ni kwamba, mwanafunzi mwenye hali hizo za moyo ni chumvi ya dunia. Lugha ya asili inasema hivi: "Ninyi – ninyi tu – ndiyo chumvi ya dunia."

Tafsiri moja na maana maishani ya mfano huu imejengwa juu ya ukweli kwamba katika siku za Yesu, hayakuwepo majokofu (au, mashine za barafu). Njia pekee ya watu kuhifadhi samaki au nyama zingine ilikuwa ni kuzipaka chumvi. Basi, Yesu hapo alikuwa anatoa tamko juu ya wanafunzi Wake na juu ya dunia, kwamba, dunia inaoza kama nyama, na wanafunzi Wake ndiyo chumvi iliyohitajika na dunia ili kuhifadhiwa kutokana na uharibifu kiadili. Njia pekee ambayo wanafunzi Wake wangeweza kuhifadhi dunia isiharibike ni "kupakwa" kwao katika watu wa dunia hii. Ule ushawishi wa "chumvi" ya tabia ya Kikristo utahifadhi dunia isipotoke na kuharibika kiadili.

Tafsiri nyingine na maana katika maisha ya kile Yesu alichomaanisha alipotumia mfano wa chumvi ya dunia hutokana na ukweli kwamba neno "mshahara" linatokana na maneno "fedha ya chumvi". Hayo maneno yanatokana na siku za Dola ya Rumi. Warumi walijua kwamba hakuna kitu hai kinachoweza kuishi pasipo chumvi. Basi, walitawala chumvi duniani kote. Walikuwa wanawalipa watumwa wao mshahara kwa kuwapa mabonge ya chumvi.

Yesu alichokuwa anawaambia wanafunzi Wake ni hiki: "Wale watu kule chini ya mlima hawana uzima. Kama ninyi mtaelewa, kuamini na kufanyia kazi haya niliyowaonyesha kwa njia ya mfano wa hali hizo nane za moyo, mtakuwa na uzima, na mtakuwa chanzo au asili ya watu hao kupata, kuhifadhi na kutokeza yaliyo bora maishani. Basi, ninyi tu ndiyo nafasi ya watu hawa kupata uzima."

Kama katika mifano yote ya Yesu, kuna maana nyingi tu maishani, tena za ajabu sana, unapotafakari na kufikiri juu yake. Chumvi huwafanya watu kuwa na kiu, na mwanafunzi huwafanya watu wa kawaida kuwa na kiu kwa ajili ya kile alichogundua ndani ya Kristo. Chumvi huumiza inapoingia katika vidonda vya watu wenye dhambi. Vivyo hivyo, maisha ya mwanafunzi wa Yesu huumiza yanapokuwa kando ya mwenye dhambi. Chumvi ina hali ya kusafisha na kuponya, na mwanafunzi anayeishi hali za moyo zilizofundishwa na Yesu ana ushawishi huo mzuri katika maisha ya wale wanaokutana naye na kujuana naye hapa duniani.

Utamaduni ni nini? Utamaduni ni neno ambalo maana yake ni, “Hivi ndivyo tunavyofanya mambo.” Yesu alikuja duniani kubadilisha utamaduni – kugeuza na kupindua utamaduni. Mkakati Wake ulikuwa kubadilisha mioyo ya watu, halafu kuwatuma wao kuingia katika utamaduni ili kugeuza utamaduni husika. Hizi sura tatu za Maandiko zimeandika mafundisho ya Yesu ambayo yalikusudiwa na yanayokusudiwa kubadilisha na kupindua dunia! Mkakati huo ni dhahiri kama tutaelewa maana ya Yesu kuwaambia wanafunzi hao: “Ninyi – ninyi tu – ndiyo chumvi ya dunia”.

Wakati mwingine waamini huwa na hali ya kujidhania kuwa ngome. Wanajificha na kutokuwa na mahusiano yoyote na wasioamini. Hatuwezi kuwa na ushawishi kama chumvi juu ya watu wa dunia hii kama sote tutakaa ndani ya “chombo cha chumvi”. Tutakuwa nao kama tutakuwa na mahusiano na watu wa dunia hii, maana ndipo tutakapowaonyesha hali za moyo wa mwanafunzi wa Kristo, kadiri Mungu anavyotupa neema ya kuishi kulingana na hali hizo za moyo.

Wakati Yesu alipowaombea mitume Wake, alimwomba Baba asiwaondoe katika dunia hii (ktk Yohana 17:15). Njia moja ya Bwana wetu kuhakikisha kwamba chumvi inaenea kila mahali ni kupitia ukweli kwamba lazima tufanye kazi ya kutunza familia zetu. Hiyo inatupa mahusiano na watu waliopotea ambao tunapaswa kuwagusa kwa hali zetu za moyo kama wa Kristo. Vile vile amefanikisha hilo katika historia ya kanisa kwa mateso.

Kuna mishenari mmoja maarufu aliyekabili hali ya “ngome” ya wamishenari wake katika nchi ya kigeni kwa kusema hivi: “Wamishenari ni kama mbolea. Wanapokuwa pamoja wananuka, lakini ukiwasambaza, wanafanya kitu kizuri.”

Je, wewe ni chumvi ya dunia, kwa neema ya Mungu? Je, muujiza kwamba Kristo amekupa hali hizo za moyo hubadilisha watu unaokutana nao? Kama unakiri kwamba ni mwanafunzi wa Yesu, na kama muujiza huo si kitu halisi maishani mwako, kuna onyo la kutisha kabisa hapa. Kulingana na Yesu, ni hivi: hufai kwa lolote! Unapaswa kutupwa nje na kukanyagwa. Hili ni neno moja la Yesu ambalo ni gumu sana.

Hiyo mifano miwili ya chumvi na nuru pia inategemeana na ukweli kwamba wanafunzi wa Yesu wamebadilishwa. Kusugua nyama kwenye nyama hakuwezi kuizuia isioze. Mwanafunzi ambaye ni chumvi lazima awe tofauti na watu anaowashawishi. Maana nyingine ya mfano huu ni kwamba mwanafunzi aliye chumvi huwafanya wengine kuwa na kiu ya kutaka kuwa kama yeye, na kupata alicho nacho ndani ya Kristo. Ili kuwa na matokeo kama hayo kwa watu, lazima tuwe tumebadilishwa na tuwe tofauti. Yesu atauliza swali lifuatalo mwisho wa sura hii: “Je, mnafanya nini kuliko wanachofanya wengine?” (ms. 47). Hali za moyo ambazo Yesu anatamka hapa zinaonyesha hiyo tofauti na kutoa jibu kwa swali Lake.

Nuru Ya Dunia

Mfano wa pili nao unasema kitu kuhusu mwanafunzi Wake na kuhusu dunia. Katika lugha ya asili, maneno ni haya: “Ninyi – ninyi tu – ndiyo nuru ya dunia.” Wakati Yesu alipowalilia makutano, kilichomgusa kuwa na huruma kuliko kitu kingine chochote ni kwamba walikuwa kama kondoo wasiokuwa na mchungaji (ktk 9:36). Hawakujua upande wao wa kuume, wala wa kushoto. Hawakuwa na nuru. Kama ambavyo wanafunzi walikuwa ndiyo chumvi pekee yenye kuweza kutoa au kuhifadhi uhai, wao ndiyo chanzo pekee cha nuru kwa ajili ya kundi lile la watu.

Mwishoni mwa huduma Yake ya miaka mitatu kwa watu wote, Yesu aliomba sala Yake kama Kuhani Mkuu, iliyoandikwa katika sura ya kumi na saba ya Injili ya Yohana. Katika sala hiyo, Yesu anataja dunia mara kumi na tisa. Kweli, dunia ilikuwa moyoni Mwake! Lakini, aliomba hivi: “Siiombei dunia, bali naomba kwa ajili ya wale ulionipa. Dunia haijui, lakini Mimi nimewapa wanafunzi Wangu Neno Lako, nao wanajua” (ktk Yohana 17:9, TLR).

Nuru pekee katika dunia hii itatoka kwa wanafunzi Wake. Kama ambavyo chumvi haiwezi kushawishi dunia ikiwa katika chombo cha kuwekea chumvi mezani, wanafunzi Wake wanapaswa kwenda mahali ambako ni giza, na kuiruhusu ile nuru tuliyo nayo kwa neema ya Mungu, ing’ae katika hilo giza. Kama wewe ndiye mwamini pekee katika familia yako, au kazini pako, au katika eneo lako, au katika kijiji chako au chuoni kwako, kumbuka kwamba mshumaa mmoja una thamani sana gizani, kuliko mshumaa mmoja ulioko katikati ya mingine. Kama wewe ndiye mwamini pekee, jua kwamba umewekwa hapo katika hilo giza kwa mpango kamili, nawe peke yako ndiye nuru katika dunia ya wale wanaokujua.

Yesu anapoagiza kwamba, “Iache nuru yako ing’ae mbele za watu, wapate kuyaona matendo yako mema na kumtukuza Baba yako aliye mbinguni”, anajua watatambua kwamba bila shaka Yeye ndiye aliwasha mshumaa wako maana usingeweza kuwa na kufanya yale wanayoyaona katika maisha yako (Mathayo 5:16).

Mshumaa Kwenye Kinara

Huu ni mfano wa ajabu sana. Yesu anatoa tafsiri na maana katika maisha anaposema kwamba, mshumaa unapowashwa ndani ya nyumba, hauwekwi chini ya kapu bali juu ya kinara. Basi, hatupaswi kuweka ushuhuda wetu chini ya kikapu, mahali ambapo hauna nguvu yoyote juu ya giza.

Haiwezekani mshumaa kutoa nuru bila ya kuteketea. Njia pekee ya mshumaa kujiokoa ni kuzima nuru yake. Yesu anachofundisha hasa ni hiki: “Kabla ya kuwa mmoja wa wanafunzi Wangu, ulikuwa kama mshumaa usiowashwa. Lakini sasa kwa kuwa

umeshapitia hayo yote yanayohusika kukufanya Mkristo, mshumaa wako umewashwa. Mimi nimewasha maisha yako, na kila niwashapo mshumaa, nina kinara nilichokichagua, ili huo mshumaa ukae hapo."

Mwisho wa miaka ile mitatu aliyokaa nao, Yesu aliwaambia hivi mitume Wake, "Ninyi hamkunichagua Mimi, bali Mimi niliwachagua ninyi na kuwateua mwende na kuzaa matunda – matunda yatakayodumu" (ktk Yohana 15:16, TLR). Neno la Kiyunani lililotafsiriwa "kuteuliwa" maana yake "kuwekwa mahali kwa mpango maalum". Neno hilo linapatikana mara tatu tu katika Biblia. Kihalisi ni kwamba, Yesu alikuwa anasema hivi, "Mimi nimewachagua ninyi makusudi, na kuwapangia mahali ambapo mtazaa matunda."

Je, umewahi kumwona kobe akiwa juu ya nguzo? Kila unapomwona kobe juu ya nguzo, uwe na uhakika mmoja kuhusu huyo kobe – hakufika hapo mwenyewe. Lazima kuna mtu kamweka kwa sababu kobe hawawezi kupanda nguzo! Kila mfuasi wa kweli wa Kristo anatakiwa kujisikia kama kobe kwenye nguzo. Wote tunapaswa kutazama hapa na pale – kila mahali – na kutambua mahali tulipowekwa kwa mpango kamili hapa duniani, na, tukimkumbuka kobe kwenye nguzo, tuseme hivi: "Nisingeweza kuwa hapa nilipo kama Kristo hakuniweka hapa."

Mji Kwenye Mlima

Mfano wa nne ni huu: "Mji uliowekwa juu ya mlima hauwezi kufichika" (ms. 14, TLR). Hapa, Yesu anarudia kwa ajili ya kukazia fundisho Lake kwamba, tukiwa na zile hali nane za moyo katika maisha yetu, hatuwezi kuzificha, kama ambavyo hatuwezi kuficha mshumaa katika kapu. Kwa kweli, hakuna mwanafunzi wa siri wa Yesu Kristo. Yesu anafanya hilo lisiwezekane wakati anapowaagiza wanafunzi Wake kumbatiza kila mtu anayekiri kwamba ni mwanafunzi Wake (ktk Mathayo 28:18-20).

Hapa, Yesu anafundisha kwamba kama sisi ni chumvi ya dunia na nuru ya dunia, hatutaweza kuficha uhalisi huo uliobarikiwa. Yesu alikuwa mkweli kabisa. Yeye alithamini sana utendaji kuliko maneno tu. Hiyo mifano minne inakazia ukweli wa jinsi tulivyo,

kuliko tunavyosema. Sisi ni chumvi, ni nuru, ni mshumaa na ni mji juu ya mlima. Marko anatuambia katika Injili yake kwamba watu walikuwa na shauku sana ya kuwa karibu na Yesu kiasi kwamba ilibidi atafute mahali pa peke yake ili aweze kuwa na wakati na Mungu kwa sababu jinsi alivyokuwa isingeweza kufichika (ktk Marko 7:24).

Katika zile hali za moyo, Yesu alituambia tutazame ndani. Katika hii mifano, anachotuambia ni hiki: "Sasa tazameni nje. Tazameni dunia inayowazunguka na kufikiri kuhusu changamoto iliyoko wakati aina ile ya tabia inayozalishwa ndani yenu kwa neema yangu itakapogusa utamaduni unaoharibika, utamaduni usiokuwa na uhai, na utamaduni ulio gizani".

Sura Ya Nne

"Haki Yenye Kuhusiana"

(Mathayo 5:17-48)

"Msifikiri kwamba nilikuja kuharibu Torati au Manabii. Sikuja kuharibu bali kutimiza. Kwa sababu, nawaambia hakika, mpaka mbingu na nchi vitakapopita, hakuna yodi moja wala nukta itakayopita kwenye Torati mpaka yote itimizwe. Kwa hiyo, yeyote anayevunja sheria mojawapo katika zilizo ndogo kabisa na kuwafundisha watu kufanya hivyo, ataitwa mdogo katika ufalme wa mbinguni; lakini yeyote atakayezitenda na kuzifundisha, ataitwa mkuu katika ufalme wa mbinguni.

"Kwa sababu nawaambieni, kwamba, haki yenu isipozidi hai ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia katika ufalme wa mbinguni kamwe" (5:17-20, TLR).

Sasa tunafikia sehemu ndefu na ngumu sana katika Mahubiri ya Mlimani (Mathayo 5:17-48). Sehemu hii inaanza kwa Yesu kutoa

tamko lenye nguvu sana juu ya mwelekeo Wake kwa habari ya Torati ya Mungu na haki binafsi. Watu wengine hufikiri – kwa makosa tu – kwamba Yesu alikuwa anapingana na Musa katika mistari hii. Kwa hiyo wanauliza hivi: “Kwa nini kusoma Agano la Kale, ikiwa Yesu alilifanya la zamani batili?” Yesu hakulifanya Agano la Kale kuwa batili. Wala hakuwa anapingana na Musa katika mistari hii. Yeye alikuwa anakabiliana na mafundisho ya Waandishi na Mafarisayo.

Yesu anapotaja “Torati na Manabii” anamaanisha kile tunachoita sisi “Agano la Kale”. Kimsingi, alikuwa anawaambia wanafunzi Wake hivi: “Kila kitu ninachowafundisha ninyi kinapatikana katika Neno la Mungu, lakini ninachofundisha kinapingana na yale ambayo viongozi wenu wa dini wamekuwa wakifundisha.” Vile vile ni kama alikuwa anasema hivi kwa wanafunzi Wake: “Mtakaposhuka chini kule na kuishi miongoni mwa hao watu, kama mnataka kuwa sehemu ya ufumbuzi na majibu Yangu, lazima mwelewe jinsi ya kulitumia Neno la Mungu katika maisha ya watu hao.”

Anaanza kwa kutangaza kwamba Yeye hakuja kuitangua Torati ya Mungu, na kwamba kila kitu alichokuwa anafundisha kilikuwa kinakubaliana na kulingana na kutimiza Torati ya Mungu. Katika mistari ishirini na nane inayofuata, atafafanua tamko Lake la kwanza, kuhusu tofauti ya jinsi Yeye anavyolitazama Neno la Mungu na mafundisho ya waandishi na Mafarisayo. Kiini cha tofauti hiyo kiko kwenye madai ya Yesu kwamba, amekuja kuitimiza Torati ya Mungu, na kwamba kila herufi ya maneno ya Kiebrania katika Torati itatimizwa kupitia mafundisho Yake.

Mtume Paulo atataja tofauti hiyo kuwa ni “roho ya Torati” kinyume cha “andiko la Torati” (ktk 2Wakor. 3:6). Paulo anaandika kwamba roho ya Torati hutoa uzima, lakini herufi ya Torati inaua. Roho ya Torati inatoa uzima kwa sababu roho ya Torati ni upendo. Roho ya Torati inatukumbusha kwamba Torati yote ya Mungu – au Neno la Mungu – ilizaliwa katika moyo wa upendo wa Mungu kwa mwanadamu. Siku zote Yesu alikuwa na mtazamo huo.

Yesu alitimiza kusudi la Torati – au Neno la Mungu – kwa kuitafsiri na kutumia roho ya Torati kila wakati. Njia nyingine ya kusema hayo ni kusema kwamba, alipitisha Torati ya Mungu katika "kioo" cha upendo wa Mungu kabla ya kuifanyia kazi katika maisha ya watu wa Mungu. Waandishi na Mafarisayo, aidha hawakujua walipaswa kufanya hivyo, au walisahau kwamba Torati ya Mungu ilikuwepo kwa ajili ya faida ya watu wa Mungu. Waliwaharibu watu wa Mungu kwa jinsi walivyofanyia kazi andiko la Torati – au Neno la Mungu – katika maisha ya watu wa Mungu.

Yesu akasema kwamba haki binafsi, au maisha yaliyo sawa ya wanafunzi Wake lazima yazidi haki ya waandishi na Mafarisayo. Anaonya kwamba mwanafunzi Wake yeyote atakayevunja amri iliyo ndogo kabisa katika amri za Mungu na kuwafundisha wengine kufanya hivyo, atakuwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni. Anatangaza kwamba wanafunzi Wake <u>wasipofanya</u> na kufundisha zile amri za Torati, hawatakuwa wakuu katika ufalme aliokuwa anazungumzia katika mafundisho Yake.

Wakati Yesu anatoa maana ya maisha katika mafundisho Yake kuhusu zile hali za moyo (ktk 5:17 hadi 7:27), atafananisha haki anayofundisha na anayotaka wanafunzi Wake kuwa nayo, na ile "haki" ya kinafiki ya hao viongozi wa dini. Ile "haki" (na inatakiwa siku zote kuwa katika mabano) ya waandishi na Mafarisayo ilikuwa <u>ya nje,</u> lakini ile haki ya mwanafunzi wa Yesu ilitakiwa kuwa <u>ya ndani.</u> Yesu alifanya mazungumzo na hao viongozi wa dini yaliyokuwa malumbano kwa sababu wao walikazia sana matendo ya dini kwa nje, na kupuuza maswala muhimu sana ya ndani, yaliyokuwa ya moyoni (ktk Marko 7:8, 15).

Haki ya jamii ya kidini ilikuwa <u>kati ya watu.</u> Wao walikazia sana jinsi mambo yanavyoonekana – ili waonekane kuwa watu wa dini sana mbele za watu. Yalikuwa ni maonyesho yaliyofanywa kwa faida ya watu – ili waonekane wanapotoa, au wanapoomba. Lakini, kimsingi, Yesu anawafundisha wanafunzi Wake hivi: "Haki yenu haipaswi kuwa kwa watu. Inapaswa <u>kuelekezwa juu.</u> Ni lazima iwe mbele za, na kwa ajili ya Mungu." Ndiyo sababu anawafundisha wanafunzi Wake wasitende haki yao mbele ya watu (ktk 6:1).

Ile haki ambayo Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake ilikuwa ya Kimaandiko, wakati ambapo haki ya hao viongozi wa dini ilikuwa ya mapokeo kwa sehemu kubwa. Haki ya Farisayo mara nyingi haikuwa na msingi katika Maandiko, na wakati ambapo ilikuwa hivyo, haikutokana na tafsiri sahihi ya Maandiko.

Yesu anahitimisha tofauti kati ya haki aliyofundisha na ile ya jamii ya kidini anapowaita hao viongozi "wanafiki". Hili lilikuwa neno la Kiyunani lenye maana ya uso bandia uliokuwa unavaliwa na wacheza maigizo wa Kiyunani, waliokuwa sehemu ya Dola ya Kiyunani iliyokuwa kabla ya Dola ya Rumi. Wakati Yesu alipochagua jina hilo kama maelezo aliyopenda sana kuhusu hao viongozi, alikuwa anatangaza kwamba haki yao ilikuwa ya kinafiki wakati ambapo haki ya wanafunzi Wake ilitakiwa kuwa halisi – ya kweli.

Tunapoelewa kile anachosema Yesu katika mistari hii kuhusu Maandiko na haki, tutatambua ni kwa nini alikuwa na malumbano ya mara kwa mara na hao waandishi na Mafarisayo. Vile vile tutapata utangulizi wa kutusaidia katika kuelewa fungu hili gumu na refu ambalo sasa tunajifunza.

Katika mistari hii ishirini na nane, tutamsikia Yesu akisema mara sita maneno kama haya: "Imesemekana," au "Wamekuwa wakiwafundisha hivi kwa muda mrefu, lakini sasa hebu sikilizeni Neno la Mungu linavyofundisha." Mara sita atataja mafundisho ya viongozi wao wa dini, na halafu atatoa mafundisho Yake.

Kuna nyakati ambapo anapingana na jinsi viongozi wa dini wanavyotafsiri na kufafanua na kufanyia kazi Torati ya Mungu. Hapo, atatimiza Torati ya Mungu kwa kufundisha roho ya Torati. Wakati mwingine Yesu anapingana na fundisho la mapokeo yao moja kwa moja – katika Talmud – ambalo halikuwa linatokana na Neno la Mungu. Mathayo na Marko kwa pamoja wanaeleza kuhusu Yesu akiwa katika malumbano na hao viongozi kwa sababu waliweka mapokeo yao kuwa yenye mamlaka kuliko hata Neno la Mungu (ktk Mathayo 15:3-6; Marko 7:9-13).

Baada ya kusema hayo, hebu tutazame mafundisho sita ya waandishi na Mafarisayo, yanayotazamwa upya na Bwana Yesu na kurekebishwa.

Ndugu Yako

"Mmesikia kwamba zamani walisema, 'Usiue, na yeyote anayeua atakuwa katika hatari ya kuhukumiwa.' Lakini Mimi nawaambia kwamba, yeyote atakayemkasirikia ndugu yake bila sababu, atakuwa katika hatari ya hukumu. Na yeyote amwambiaye ndugu yake, 'Raka!' atakuwa katika hatari ya kufikishwa mbele ya baraza. Lakini yeyote atakayesema, 'Mpumbavu wewe!' atakuwa katika hatari ya moto wa jehanamu.

"Basi, unapoleta sadaka yako madhabahuni, na ukiwa hapo ukumbuke kwamba ndugu yako ana kitu na wewe, iache sadaka yako hapo mbele ya madhabahu, uende zako. Kwanza kapatane na ndugu yako, kisha urudi na kutoa sadaka yako" (ktk 5:21-24, TLR).

Katika Biblia nzima, kuna maneno mawili yenye kujumlisha kweli ambayo Mungu anawafundisha watu Wake. Maneno hayo ni, "Mungu kwanza!" Katika fungu hili tunapata tofauti kidogo kwa mkazo huo. Wakati Yesu anapotuonyesha jinsi ya kufanyia kazi zile hali za moyo tulizojifunza kwa ndugu zetu, au kwa waamini wengine, anafundisha hivi: "Kwanza … ndugu yako, halafu Mungu."

Yesu anaweka mkazo mkubwa sana kwenye umuhimu wa mahusiano yetu na waamini wenzetu. Kimsingi, anafundisha kwamba lazima tufanyie kazi hali ya moyo ya tano na ya sita ya mwanafunzi mwenye huruma – asiyekuwa na kitu chochote moyoni mwake bali upendo wa Mungu – kwa wale ambao tunaabudu nao, tunaokaa nao, na tunaomtumikia Kristo pamoja nao. Haturuhusiwi hata kumwendea Mungu katika ibada binafsi kama kuna chochote kilichoharibu mahusiano yetu na yule ambaye Yesu anamwita "ndugu" yetu.

Alifundisha mahali pengine kwamba, kama sisi ndiyo ndugu mwenye kitu na mwingine, lazima tupatane na ndugu yetu (Marko 11:25). Pia anafundisha jambo hili la nidhamu ya kiroho katika

mantiki ya jamii ya kiroho ambayo ni kanisa (ktk Mathayo 18:15-17).

[USHUHUDA WA MWANDISHI: Wakati fulani nilimsikia mkurugenzi wa shirika kubwa sana la wamishenari kimataifa, akiwaambia wamishenari wake: "Hatuwezi kuipata dunia kama tutapotezana sisi kwa sisi!" Kisha akawaonyesha kitabu kimoja cha kushangaza sana. Jina la kitabu hicho lilikuwa Tatizo Kuu La Wamishenari. Alipofungua ndani, kitabu hicho kilikuwa na maneno mawili tu: "Wamishenari wengine!" MWISHO WA USHUHUDA]

Labda huo ndiyo ulikuwa mzigo wa Yesu alipotoa mafundisho haya yenye nguvu sana kuhusu umuhimu mkubwa wa waamini kuanzisha na kudumisha mahusiano ya upendo.

Viongozi wa dini walifundisha kwamba, mradi hukumwua au kumdhuru ndugu yako kimwili kwa namna yoyote ile, uhusiano mliokuwa nao na ndugu yako ulikuwa unakubalika na Mungu. Yesu anakwenda kwenye kiini cha ugomvi kati ya watu wawili wa Mungu kwa kutaja jambo la hasira, lenye kusababisha ugomvi huo. Anafundisha kwamba hasira na kujisikia chuki kwa ndugu au dada zetu lazima kushughulikiwa kama tunataka kuwa na uhusiano na waamini wenzetu, unaokubalika mbele za Mungu.

Mpinzani Wako

"Kubaliana na mpinzani wako upesi, mkiwa njiani pamoja, asije akakupeleka kwa hakimu, na hakimu akakukabidhi kwa askari, nawe utupwe gerezani. Hakika nakwambia, hutatoka huko kwa njia yoyote ile mpaka utakapomaliza kulipa senti ya mwisho" (ktk Mathayo 5:25, 26, TLR).

Katika mistari ya mwisho ya sura hii, Yesu atatuonyesha jinsi ya kufanyia kazi hizo hali za moyo kuhusiana na adui zetu. Huyu "mpinzani" anaweza kuitwa siku hizi "mshindani". Tunaishi katika dunia yenye ushindani sana. Tunapofanya biashara na watu wengine, wao ndiyo wanaopata fedha, na sisi ndiyo hupata ujuzi. Huyu mpinzani ni miongoni mwa watu wanaokusudia kupata fedha yetu na kutupa sisi ujuzi.

Wakati mwingine, mahusiano yetu na hao wapinzani huwa mabaya, nao wanadhamiria kutushtaki, au hata kutufunga gerezani. Hiyo hali ya moyo ambayo Yesu anafundisha kwamba tuitumie kwa wapinzani wetu na adui zetu, ni dhahiri kabisa, kwamba, "Wamebarikiwa wanaotafuta amani." Wanafunzi wenye hali ya moyo ya saba na ya nane hawakasiriki wala kutafuta kulipa kisasi wakati wapinzani wao wanapodhihirisha uhalisi mbaya kwamba hawatutakii mema.

Ingawa hatuwezi kutawala anachofanya mpinzani, mwanafunzi wa Yesu hukubali wajibu wa kuona kwamba yeye hatahusika kuanzisha ugomvi na wapinzani. Paulo aliandika kwamba, kwa kiasi wajibu wetu unavyohusika, tuishi kwa amani na watu wote (ktk Warumi 12:18). Wajibu wetu katika mahusiano haya una mahali unapoanzia, na siku zote una mahali unapomalizikia pia. Hatuwezi kutawala – na basi hatuhusiki – kile ambacho mpinzani wetu atafanya.

Wanawake

"Mmesikia kwamba zamani walisema, 'Usizini.' Lakini Mimi nawaambia kwamba, yeyote anayemtazama mwanamke ili kumtamani, amekwisha zini naye katika moyo wake.

"Kama jicho lako la kulia linakufanya utende dhambi, ling'oe na kulitupa mbali nawe; kwa sababu kuna faida zaidi kwako kama kiungo chako kimoja kitaangamia kuliko mwili wako wote utupwe jehanamu. Na kama mkono wako wa kulia utakufanya utende dhambi, ukate na kuutupa mbali nawe; kwa sababu kuna faida zaidi kwako kama kiungo chako kimoja kitaangamia kuliko mwili wako wote utupwe jehanamu." (ktk ms. 27 hadi 30, TLR).

Kwa kuwa mafundisho haya yanalengwa kwa wanaume, tunaweza kuhesabu kwamba faragha hii ilikuwa ya wanaume tu. Bila shaka mafundisho haya yanawahusu wanawake watauwa pia wanaotaka kuwa chumvi na nuru kwa ajili ya Yesu. Tafsiri na maana yake katika maisha ni kwamba mafundisho haya yanahusu mahusiano yetu na wale wasiokuwa wa jinsia yetu.

Kama alivyofanya na hasira na mauaji, Yesu anakwenda kwenye chanzo cha dhambi ya uzinzi. Hakufundisha kwamba tamaa, au kile anachoita kuzini katika moyo wetu kuwa ni dhambi inayolingana na uzinzi halisi. Hoja Yake ni kwamba kama kweli tunataka kuwa sehemu ya ufumbuzi au majibu anayotoa – na kuwa na ushawishi wa chumvi na nuru – ni lazima tujifunze jinsi ya kuzuia tamaa zetu za kutaka mahusiano ya kimwili na watu wa jinsia nyingine.

Kama hatutaki kuzini, lazima tushinde hiyo vita kwa kushughulikia maswala yanayopelekea uzinzi – kutazama kwa kutamani, na kufikiri mawazo ya zinaa. Yakobo – ndugu Yake – anatoa ufafanuzi mzuri kuhusu dhambi katika barua yake ya Agano Jipya. Anaandika kwamba kutazama hufuatwa na tamaa sana. Tamaa huongoza kwenye kujaribiwa, ambako hufuatwa na dhambi, na dhambi siku zote huishia kwenye ile karamu ya matokeo ambayo Biblia huita “kifo” (ktk Yakobo 1:13-15; tazama pia Warumi 6:23).

Yesu na ndugu Yake – Yakobo – wanafundisha kwamba ni rahisi zaidi kushinda dhambi ya mahusiano ya kimwili na watu wa jinsia nyingine kwa kuepuka kutazama mara ya pili, na kufikiri mawazo machafu na kulea tamaa. Tunapaswa kushinda kabla tamaa yetu haijatuongoza kwenye kukabiliana na majaribu. Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake kwamba waombe kila siku ili waepuke majaribu (ktk Mathayo 6:13).

Fundisho la Yesu kuhusu kung’oa jicho letu la kulia au kukata mkono wa kulia halipaswi kufanyiwa kazi kama lilivyo. Roho ya fundisho hili ni kwamba, kama tunachotazama kinatuongoza kwenye dhambi, tunapaswa kuacha kukitazama. Ni Bwana tu ndiye ajuaye dhambi inayotendeka katika dunai yetu siku hizi kwa sababu ya watu kutazama sinema na picha mbaya, zinazowahamasisha na kuwasisimua kutamani na hatimaye kutenda dhambi za mahusiano kimwili na watu wa jinsia nyingine.

Vivyo hivyo, anafundisha kwamba kama kile tunachofanya na mkono wetu kinatupelekea kwenye dhambi, tunapaswa kuacha kukifanya. Katika mahali pengine anaweka na mguu pia, na maana yake maishani ni kwamba kama mahali miguu yetu inapotupeleka

hutuongoza kwenye dhambi, hatupaswi kwenda huko (ktk Mathayo 18:8).

Mke Wako

"Walisema pia, 'Yeyote amwachaye mke wake, ampe cheti cha kuachana.' Lakini Mimi nawaambia ninyi kwamba, yeyote amwachaye mke wake kwa sababu yoyote isipokuwa uzinzi, anamwingiza kwenye uasherati; na yeyote amwoaye mwanamke aliyeachwa na mumewe anaingia katika uasherati" (ktk Mathayo 5:31, 32, TLR).

Mafundisho yote ya Yesu hapa mlimani yanapaswa kutafsiriwa na kufanyiwa kazi huku tukikumbuka mantiki yake. Mkakati wa Yesu ni kufundisha wanafunzi ambao watatumwa ili kwenda kuwa chumvi na nuru kwa watu ambao wamelemewa na matatizo yao huko chini ya mlima. Lazima tukumbuke kwamba makundi ya watu wale yaliwakilisha dunia ya watu waliopotea.

Sulemani aliandika kwamba watoto ni kama mishale, na wazazi wao ni kama upinde ambao unawatupa katika maisha (Zaburi 127:3-5). Mambo ya thamani, makusudi na mwelekeo wa maisha ya watoto hutegemeana na upinde uliowatupa maishani. Leo hii duniani kote, Shetani anajaribu sana kukata kamba ya huo upinde. Matengano na talaka vimezidi katika tamaduni nyingi sana. Katika fungu hili Yesu anafundisha kwamba kama tunataka kuwa sehemu ya ufumbuzi au majibu Yake, lazima tufanyie kazi zile hali za moyo zilizobarikiwa kwa mahusiano yetu na wenzetu katika ndoa.

Huu ni mfano wa waandishi na Mafarisayo kutumia maneno ya Musa, lakini Yesu hakukubaliana na tafsiri yao na jinsi ya kufanyia kazi mafundisho ya Musa. Musa aliamuru kwamba, kama mtu akimwacha mke wake, "na ampe hati ya talaka" (ktk Kumbukumbu 24:1-4).

Kama Yesu alivyowaonyesha hao viongozi wa dini wakati mwingine, Musa aliruhusu hati ya talaka kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao (ktk Mathayo 19:7-8). Zamani sana katika kipindi cha Agano la Kale cha historia ya Waebrania, viongozi wa kiroho wa Kiyahudi walimtafsiri Musa kwamba alimaanisha kwamba, kama

mwanamume hakupendezwa na mke wake kwa sababu yoyote ile, aliweza kumpa talaka na kumwacha. Mume hakutakiwa kumwambia mke wake, au watu wengine, sababu ya kumwacha mkewe. Alikuwa anaweza kusema kwamba hakuwa mwaminifu kwake.

Basi Musa akaweka sheria kwamba, "Ukimwacha mke wako, lazima umpe hati ya talaka." Hiyo hati ya talaka ingetoa sababu ya kuachana huko, na kumtaka mume kufanya mpango kwa ajili ya kumtunza mke aliyekuwa anamwacha. Kwa kuwa mwanamke asingeweza kuishi katika utamaduni wa Kiyahudi bila mume, Musa alichokuwa anafanya ni kujaribu kuwalinda wanawake. Ndiyo maana alidai hati ya talaka.

Yesu hafundishi kwamba talaka inakubalika. Mungu anachukia kuachana kwa wanandoa (ktk Malaki 2:16). Yesu anafundisha kwamba kama kuna sababu kwa ajili ya kuachana, mwanafunzi Wake awe mwenye haki hata katika hili. (Yatakuwepo maelezo zaidi katika vitabu vya mbele – kuhusu Ndoa na Familia, na katika vitabu vya 1 na 2 Wakorinto.)

Neno Lako

"Mmesikia tena kwamba zamani walisema, 'Usiape kwa uongo, bali, timiza viapo vyako kwa Bwana.' Lakini Mimi nawaambia, usiape kabisa: kwa mbingu, maana ndipo kiti cha enzi cha Mungu kilipo; wala kwa dunia, maana ndipo anapoweka miguu Yake; wala kwa Yerusalemu, maana ndiyo mji wa Mfalme mkuu. Wala usiape kwa kichwa chako, kwa sababu huwezi kufanya nywele hata moja tu kuwa nyeupe au nyeusi. Lakini, 'Ndiyo' yako na iwe 'Ndiyo', na 'Hapana' iwe 'Hapana'. Kwa sababu, mengine yanayozidi hayo yanatoka kwa yule Mwovu" (ktk Mathayo 5:33-37, TLR).

Sasa tunarudi kwenye fundisho la viongozi wa kiroho Wayahudi ambalo halikuwa katika Torati ya Mungu. Katika mapokeo yao, walikuwa na utaratibu mrefu sana kuhusu viapo vilivyokuwa vinawafunga, na viapo ambavyo havikuwa vinawafunga (Mathayo 23:16). Wangesema hivi: "Ninaapa kwa Hekalu," au, "Ninaapa kwa dhahabu ya Hekalu". Au, "Ninaapa kwa madhabahu,"

au, “Ninaapa kwa dhabihu iliyoko madhabahuni.” Walikuwa wanaaapa kwa mbingu, au wangeapa kwa dunia, au kwa Yerusalemu.

Waliokuwa katika kundi lao walijua wakati ambapo viapo hivyo vilikuwa vinawafunga, na wakati ambapo havikuwa vinawafunga. Watu wa kawaida ambao hawakuelewa hizo tofauti kubwa wangeshangazwa sana kugundua kwamba kile walichofikiri wao kwamba ni makubaliano kamili hakikuwa makubaliano yoyote.

Huu mfumo ulikuwa na taratibu nyingi kiasi kwamba ulikuwa upuuzi. Hili lilikuwa kinyume kabisa na amri kwamba hatupaswi kushuhudia uongo. Ndiyo maana Yesu alibomoa upuzi huo wote kwa tamko Lake moja tu kwamba chochote zaidi ya “ndiyo” au “hapana” yako ilikuwa kutoka kwa Shetani! Roho ya fundisho hili ni kwamba, wanafunzi Wake lazima wajulikane kuwa watu wa Neno, na kwamba ni watu wanaotunza neno wanalosema.

Watu Waovu

“Mmesikia kwamba zamani walisema, ‘Jicho kwa jicho, na jino kwa jino.’ Lakini Mimi nawaambia, msipingane na mtu mwovu. Ila yeyote atakayekupiga kofi upande wa kulia, mgeuzie na upande wa kushoto pia. Kama mtu yeyote anataka kukushtaki ili akunyang’anye joho lako, mwachie na mgolole wako pia. Na mtu akikulazimisha uende maili moja, nenda naye maili mbili. Mpe kila anayekuomba, wala mtu anayetaka kuazima kitu kwako, usimfukuze” (ms. 38-42, TLR).

Hapa tena Yesu anakwenda kinyume na jinsi waandishi na Mafarisayo walivyotafsiri na kufanyia kazi Torati ya Musa. Hawa viongozi wa dini walikuwa wakifundisha “jicho kwa jicho, jino kwa jino”. Hayo utayakuta katika Kutoka, Walawi na Kumbukumbu la Torati. Lakini, Yesu anatangaza hivi: “Mimi sikubaliani na roho ya Torati wanayofundisha ‘jicho kwa jicho, na jino kwa jino’.”

Kama alivyofanya aliporuhusu kile cheti cha talaka, wakati Musa alipoagiza kwamba “jicho kwa jicho, na jino kwa jino,” alikuwa anaweka mipaka kwa ajili ya mioyo migumu ya watu wakorofi, wasiowezekana. Alikuwa anaweka mipaka kwa ajili ya

shauku yao mbaya ya kutaka kulipiza kisasi. Kama mtu angemtoa mwingine jino, hali yao moyoni ilikuwa hivi, “Nitakuvunja shingo!” Kama mtu fulani angewatoa jicho, hali yao moyoni ilikuwa hivi, “Nitakutoa kichwa!”

Hiyo si haki, bali ni tamaa mbaya ya kutaka kulipiza kisasi. Haki ingekuwa jicho kwa jicho, na jino kwa jino. Mara nyingi hii roho ya kutaka kulipiza kisasi ndiyo inasababisha watu kushtakiana mahakamani. Basi, Yesu anazungumzia jinsi tunavyotakiwa kufanyia kazi hali zake za moyo wakati tunapopelekwa mahakamani na kushtakiwa. Tunaposikia katika nchi kama Marekani – jinsi watu wanavyopelekana mahakamani na kudaiana mamilioni ya dola – ni dhahiri kwamba hao watu wanakwenda mbali kuliko kwenye kutafuta haki – ni kwamba wanatafuta kulipa kisasi au kujipatia bila kutokwa jacho. Maisha yetu yangekuwaje, na mahakama zetu, na ulimwengu wa kisheria katika tamaduni zetu, kama tungetilia maanani mafundisho hayo ya Yesu?

Yesu alikuwa anatimiza na kwenda zaidi ya roho ya Torati ya Musa alipofundisha hivi: “Lakini Mimi nawaambia, msishindane na mtu mwovu.” Yeye anafafanua hilo tamko na bila shaka anafanyia kazi zile hali za moyo za waleta amani wanaoteswa wakati anapowashauri wanafunzi Wake kugeuza shavu la pili, kutoa joho lao pia wanaposhtakiwa kudaiwa mgolole wao, kwenda maili ya ziada, kutoa kwa ukarimu na kutokataa kumkopesha mtu anapohitaji mkopo. Je, Yesu alikuwa anafundisha nini katika mistari hii migumu sana?

[USHUHUDA WA MWANDISHI: Nilipomwuliza mfanya biashara mmoja mambo yakoje katika ulimwengu wa biashara wenye ushindani sana, alijibu hivi: “Hatuchukui mateka wa vita, na kila aliyejeruhiwa anauawa!” Kuna mstari katika shairi moja unaosema hivi: “Asili yote ni nyekundu - ina meno na kucha.” MWISHO WA USHUHUDA]

Maisha yanaweza kuwa kama ugomvi wa mbwa – yenye ushindani mkubwa sana mpaka inaonekana ni kama mashindano ya panya. Lakini, ni “ugomvi wa mbwa” na ni “mashindano ya panya” kama sisi ni “mbwa” na “panya”. Yesu alikuwa anafundisha

kwamba, wanafunzi Wake wanapoishi kwa kulingana na zile hali nane za moyo alizofundisha, katika mahusiano yao na watu wa dunia hii, watawaonyesha watu wa dunia hii kwamba si lazima mambo yawe hivyo.

Katika siku zile, Warumi waliokuwa ndiyo watawala wangeweza kumwamuru Myahudi awabebee mzigo wao kwa kilomita kadhaa. Ilibidi watii wakiambiwa hivyo, lakini hawakulazimika kukubaliana na hiyo hali mbaya ya moyo. Yesu anafundisha hivi: "Wakikulazimisha kwenda kilomita moja, wewe nenda mbili." Katika siku za mwanzo wa kanisa, askari wengi sana wa Kirumi waliokoka kwa sababu wanafunzi wa Yesu waliokuwa makini waliishi kulingana na hali hizo za moyo walizofundishwa, katika mahusiano yao na hao bwana zao.

Adui Yako

"Mmesikia kwamba zamani walisema, 'Mpende jirani yako na umchukie adui yako.' Lakini Mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, wabarikini wanaowalaani, watendeeni mema wale wanaowachukia, na waombeeni wale wanaowatumia vibaya na kuwatesa, ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa sababu, Yeye hufanya jua Lake lichomoze juu ya waovu na wema, na hutuma mvua kwa wenye haki na wasio haki.

"Maana, mkiwapenda wale wanaowapenda tu, mna thawabu gani? Mbona hata watoza ushuru wanafanya hivyo hivyo? Na mkiwasalimu ndugu zenu tu, mnafanya nini kuliko wengine? Mbona hata watoza ushuru wanafanya hivyo hivyo? Kwa hiyo, mwe wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (ms. 43-48, TLR).

Hiyo mistari sita ndiyo migumu sana katika mafundisho ya Yesu, kuitafsiri na kuifanyia kazi. Kanisa halijawahi kukubaliana maana yake, na jinsi ya kuifanyia kazi. Inafundisha maadili ya hali ya juu sana kuliko yaliyowahi kusikika duniani.

Kwa mara ya sita katika sura hii, Yesu anaanza fundisho kwa kutaja kile ambacho waalimu wa dini wamekuwa wakifundisha. Wakati huu Yesu anafundisha hivi: "Mmesikia kwamba zamani

walisema, ‘Mpende jirani yako na umchukie adui yako’.” Nusu ya maneno hayo yalitoka kwa Musa, na nusu ilikuwa nyongeza ya mafundisho yao yaliyotokana na mapokeo. Musa aliagiza hivi: “Mpende jirani yako” (ktk Walawi 19:18), lakini hakuagiza kwamba, “Mchukie adui yako.” Katika Zaburi, tunamkuta Daudi ambaye alikuwa mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu, akituambia kwamba anawachukia adui wa Mungu. Lakini katika Neno la Mungu hatuagizwi kuwachukia adui zetu.

Tunaposoma mistari kumi na moja ya mwisho katika sura hii, ni muhimu sana kukumbuka kwamba haya mafundisho katika “Faragha ya Kikristo ya Kwanza” hayakutolewa kwa wale waliokuwa chini ya mlima. Yesu alitoa mafundisho haya kwa wale waliokuwa wanasema, kwa kuwepo kwao hapo mlimani, kwamba wao walikuwa wanafunzi wa Yesu. Ukweli kwamba wanaitwa “wanafunzi” unamaanisha kwamba walikuwa na kiwango cha juu sana cha kujitoa kwa Yesu walipofika kwenye hiyo faragha.

Hicho ndicho kiini cha kujitoa kikamilifu ambako Yesu alitaka kutoka kwa mwanafunzi: “Ukitaka kunifuata, lakini hauko tayari kujitwika msalaba wako na kufa kwa ajili Yangu, huwezi kuwa mwanafunzi Wangu. Kama hauko tayari kuniweka Mimi kwanza, mbele ya watu wote maishani mwako – mume, mke, baba, mama, watoto, wazazi – huwezi kuwa mwanafunzi Wangu. Kama hauko tayari kuacha kila kitu ulicho nacho, huwezi kuwa mwanafunzi Wangu” (ktk Luka 14:25-35, TLR).

Wale waliohudhuria faragha hii walikuwa wamefanya maamuzi hayo ya kujitoa kwa Yesu. Walikuwa wamemwambia Yesu kwamba wako tayari kujitwika misalaba yao na kumfuata. Bila shaka walikuwa wameona wafungwa wa Kirumi waliokuwa wanakwenda kusulubiwa, wakibeba misalaba yao kwenda mahali pa kuuawa. Walijua maana ya huo mfano mzito sana. Wakati Yesu alipotoa mafundisho hayo katika mistari hiyo sita, alichokuwa anawaambia ni sababu, mahali na jinsi ya kuubeba huo msalaba waliokuwa wameahidi kuubeba, wanapomfuata.

Haya mafundisho ya Yesu pia yanapingana na jinsi hawa viongozi wa kiroho walivyokuwa wanatafsiri na kufanyia kazi Torati

ya Musa. Je, unakumbuka lile swali ambalo lilitoka kwa mwanasheria, lililomfanya Yesu kutoa Mfano wa Msamaria Mwema? Swali lilikuwa: “Jirani yangu ni nani?” (ktk Luka 10:29). Lilikuwa swali zito sana kwa sababu, kulingana na maadili ya mapokeo yao, yaliyofundishwa na waandishi na Mafarisayo jirani yako alikuwa Myahudi mwenzako, lakini kila asiyekuwa Myahudi duniani kote alikuwa adui yako. Halafu, walikuwa wanatoa hitimisho hivi: Mpende Myahudi mwenzako, lakini wachukie watu wengine wote.

Tafadhali ona sababu ya kuwapenda adui zetu. Ni “Ili mwe watoto wa Baba yenu aliye mbinguni.” Hiyo ndiyo baraka ambayo Yesu aliahidi kwa wale watakaoishi kulingana na hali ya moyo ya saba na ya nane aliyofundisha Yesu, kama watoa amani wanaoteswa.

Kuna kanuni nyingine moja hivi ya kujikabidhi ambayo lazima iwepo kama tunataka kuyachukua mafundisho haya ya Yesu kwa uzito. Tukisoma mistari hiyo na kusema, “Tukifanya hivyo, tutapoteza kila kitu,” basi mafundisho hayo hayatakuwa na maana yoyote kwetu. Lazima tutambue kwamba kujiokoa si kanuni kubwa sana katika maadili ya mwanafunzi wa Yesu Kristo.

Mtume Paulo alielewa jambo la kujikabidhi kama mwanafunzi alipoandika hivi: “Nimesulubiwa pamoja na Kristo. Si mimi ninayeendelea kuishi, bali Kristo anaishi ndani yangu, na maisha ninayoishi sasa katika mwili ninaishi kwa imani katika Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yangu” (ktk Wagalatia 2:20, TLR).

Nini maana ya kusulubiwa pamoja na Kristo? Maana yake ni kuwa tayari kubeba msalaba wetu na kumfuata. Wakati Yesu alipokabiliana na msalaba Wake Mwenyewe, alisema hivi: “Mbegu ya ngano isipoanguka katika udongo na kufa, inabaki kuwa mbegu ya ngano tu. Inapokufa na kuzikwa, ndipo inazaa matunda.” Halafu akaomba hivi: “Baba, nafsi Yangu inasumbuka sana. Nami nisemeje? ‘Niokoe na saa hii?’ Hapana, maana nilikuja duniani kwa sababu hii.”

Basi anafikia kuomba hivi: “Baba, jitukuze Mwenyewe.” Sauti ikatoka mbinguni na kujibu hivi: “Nimekwisha fanya hivyo,

nami nitafanya hivyo tena" (ktk Yohana 12:23-28, TLR). Katika mantiki ya wakati huo mgumu, Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake kuungana Naye katika kukubaliana na kujitoa kikamilifu ambako Yeye anawaonyesha kwa njia ya mfano, alipokabiliana na msalaba Wake Mwenyewe (ktk Yohana 12:25, 26).

Mchungaji mmoja mcha Mungu alishauri kila mwanafunzi wa Yesu kuomba sala hiyo ya Yesu, iliyorekebishwa hivi: "Baba! Jitukuze Mwenyewe na unitumie Mimi gharama. Chochote Baba. Wewe jitukuze Mwenyewe tu!" Tunapoungana na Bwana wetu katika sala aliyoomba alipokuwa anakabiliwa na msalaba Wake Mwenyewe ndipo tutaelewa, kukubali na kufanyia kazi maadili ya hali ya juu sana ambayo dunia hii imewahi kusikia.

Wakati wa Vita Takatifu, Francis wa Asisi alikuwa anamtunza Mturuki mmoja aliyejeruhiwa. Mpiganaji mmoja Mkristo akapita akiwa juu ya farasi na kusema, "Wewe Francis! Huyo Mturuki akipona, atakuua!" Francis alijibu hivi, "Sawa tu. Atakuwa amefahamu upendo wa Mungu kabla hajafanya hivyo!"

Ona jinsi ambavyo Yesu anamalizia mafundisho hayo. "Kwa hiyo, mwe wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu" (ms. 48, TLR). Neno hilo "mkamilifu" halimaanishi ukamilifu bila dhambi. Maana yake ni, "Mwe watu waliokomaa, wakamilifu, jinsi ambavyo Mungu aliwaumba kuwa katika kila kitu." Ikiwa neno "mkamilifu" linakusumbua, liondoe katika sentensi hiyo yote. Utaona kwamba, kama hitimisho la mafundisho Yake yote kuhusu roho ya Torati, Yesu anafundisha kwamba sisi tunapaswa kuwa kama Baba yetu wa mbinguni alivyo. Yesu anafundisha kwamba, sisi kama watoto wa Mungu tunapaswa kuwa kama Baba yetu, Mungu. Yeye yukoje kwani?

Mtume Paulo anawashauri waume kuwapenda wake zao kama Kristo alivyolipenda kanisa wakati alipojitoa kwa ajili yake (ktk Waefeso 5:25). Wakati Paulo anapoagiza hao waume kupenda, kama Kristo alivyopenda na anavyopenda, na kutoa kama Yeye alivyotoa na anavyotoa, kwa kweli anafundisha kitu kile kile ambacho Yesu anafundisha hapa – kwamba tuwe kama Kristo alivyo. Je, hayo yanawezekana?

Nini fundisho lenye nguvu kuliko yote katika Agano Jipya? Ni hili: “Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.” Paulo ni kama aliandika hivi: “Mimi nimeinuliwa na Mungu ili kulishirikisha kanisa siri. Na hiyo siri ni hii: Kwamba, Kristo ndani ya mioyo yenu ndiye tumaini pekee mlilo nalo” (ktk Wakolosai 1:27, TLR).

Haya mafundisho ya kiadili ya Yesu hayawezekani kabisa – tena, ni kituko kikubwa – isipokuwa muujiza huu mkubwa uwe umefanyika na kukamilika kwako: “Kristo ndani yako, na wewe ndani ya Kristo.” Tena, “pamoja Naye.” Lakini fundisho lenye nguvu sana katika Agano Jipya liko mahali pake tayari! Basi, tunaweza kulichukua fundisho hilo kwa dhati kabisa na kuthubutu kujibu maswali haya: “Je, Yesu alisema nini? Alimaanisha nini?” Na swali lingine: “Nini maana yake kwangu?”

Mstari wa ajabu sana katika fungu hili la kushangaza la Maandiko unakubaliana na mkakati na lengo la utume wa Yesu, anapoendesha faragha hii. Yesu aliuliza swali hili: “Mnafanya nini cha zaidi kuliko wengine?”

Kama tulivyokwisha ona mapema, chumvi lazima iwe tofauti na nyama inayosuguliwa nayo ili kuihifadhi isiharibike. Tafsiri moja inasema hivi: “Kama ninyi mnawapenda wale tu wanaowapenda, ni neema gani mnayotenda hapo?” (Mathayo 5:46). Maana yake ni kwamba hakuhitajiki neema yoyote kuwapenda wanaotupenda, lakini inahitajika neema ya Mungu kuwapenda wale ambao ni adui zetu.

Fungu hili gumu – au sura hii nzima – hutupa sisi changamoto kwa swali hili: “Je, kuna chochote katika maisha yetu kinachoweza kuelezwa kwa ile siri ya kiroho kwamba, Bwana wetu Yesu Kristo, aliyefufuka, anakaa ndani ya mioyo yetu?”

Sura Ya Tano

"Nidhamu Kiroho Na Thamani Za Juu"

(Mathayo 6:1 – 34)

Mpaka hapa Yesu ametoa changamoto kwa wanafunzi Wake watazame ndani na kufikiri juu ya zile hali za moyo zilizobarikiwa, zinazopaswa kuwa mioyoni mwao (5:3-12). Halafu akawahimiza watazame pembeni na kufanyia kazi hizo hali za moyo katika mahusiano yao (5:13-48). Anapomaliza kuwafundisha jinsi hizo hali za moyo zinavyotakiwa kufanya kazi katika mahusiano yao – hasa kwa wapinzani wao, watu waovu, na adui zao – walikuwa tayari kwa ajili ya kile alichofundisha baada ya hapo.

Sura ya sita inasimulia habari za Yesu akiwaelekeza wanafunzi Wake kutazama upande mwingine. Sasa anawahimiza wanafunzi Wake kutafuta nguvu ambayo wameamini wanaihitaji, kwa kutazama juu. Kwa kuwa mwanafunzi – kwa maana ya neno lenyewe –a mekwisha fanya uamuzi wa kujitoa na kuwa mwenye nidhamu, sasa anawaelekeza kwenye utaratibu wa kila siku wa kutazama juu kwa kuwafundisha umuhimu wa kuishi maisha yao kwa nidhamu za kiroho, au thamani za juu na zenye maana.

Nidhamu Ya Kiroho Ya Kutoa

"Mwe makini msitende 'matendo ya haki' mbele ya watu, ili mwonekane nao. Mkifanya hivyo, hamtakuwa na thawabu kutoka kwa Baba yenu wa mbinguni.

"Basi, mnapotoa kwa wenye kuhitaji, msitangaze kwa matarumbeta, kama wanafiki wanavyofanya katika masinagogi na mitaani, ili kuheshimiwa na watu. Ngoja niwaambie ukweli. Wao wamekwisha pokea thawabu yao yote. Lakini mnapotoa kwa wahitaji, msikubali mkono wa kushoto ujue kinachofanywa na mkono wa kulia, ili kutoa kwenu kuwe kwa siri. Ndipo Baba yenu, anayeona mambo yote yanayofanyika kwa siri, atakapowapa thawabu" (ktk 6:1-4, TLR).

Tumeona kwamba “haki” ya waandishi na Mafarisayo ilikuwa kuelekea watu, wakati ambapo haki aliyokuwa anafundisha Yesu na kudai wanafunzi Wake wawe nayo ilikuwa yenye kuelekea juu. Mistari minne ya kwanza ya sura hii ya sita inaeleza vizuri sana tofauti hiyo. Ingawa tunaweza kuona shida kufikiri hivyo siku hizi, Mafarisayo walikuwa wanabeba tarumbeta ndogo katika makanzu yao, na kabla ya kudondosha fedha katika chombo cha maskini, walikuwa wanaipiga. Walitaka watu waone utoaji wao na kuwaheshimu kwa kuwa watauwa na wakarimu.

Yesu aliandika neno Lake maarufu sana kwa ajili yao kuhusu tendo hilo: “Wanafiki!” Kama wale waigizaji wa Kiyunani, Mafarisayo walikuwa wanavaa uso bandia na kujifanya tu walipokuwa wanatoa kwa namna hiyo. Bila shaka walikuwa wanatenda haki yao mbele ya watu – ili waonekane na kuheshimiwa na watu – kitu kilichomfanya Yesu kutoa maagizo hayo kwa ajili ya nidhamu ya wanafunzi Wake katika utoaji. Maagizo yake ni kwamba wanafunzi Wake watoe kwa siri – pasipo hata mkono wa kushoto kujua kinachofanyika na mkono wa kulia.

Hawa wanafiki walipopokea sifa za wanadamu, walikuwa wamekwisha pokea thawabu pekee ambayo wangepata kwa ajili ya utoaji wao. Wanafunzi wa Yesu wanapaswa watoe kwa siri kwa Mungu anayeona kinachotolewa kwa siri. Yeye atawapa thawabu waziwazi kwa ajili ya utoaji wao wa siri na wa utauwa – ambao kwa kweli ndiyo kiini cha imani na kuabudu. Sura ya imani katika Biblia inatuambia kwamba yeye amwendeaye Mungu na atakaye kumpendeza Mungu sharti aamini kwamba Mungu yupo, na kwamba anawapa thawabu wale wanaomtafuta kwa bidii kwa sababu wanaamini yupo (ktk Waebrania 11:6).

Kabla hatujawa wakali sana katika kuwalaumu Mafarisayo hawa, lazima tujiulize sisi wenyewe ikiwa hatupulizi tarumbeta kwa namna moja au nyingine tunapotoa kwa jinsi ambavyo watu wanafahamu tumetoa nini. [USHUHUDA WA MWANDISHI: Mimi kama mchungaji nimegundua kwamba watu wanaotoa sadaka kubwa mara nyingi wanafanya hivyo kwa njia ambayo mchungaji na wakati mwingine kanisa zima hutambua kilichotolewa. Nimewahi

kuambiwa kwamba ni jambo zuri sana kutoa sadaka kubwa kwa siri – halafu watu wagundue! MWISHO]

Lazima tuseme kwamba nidhamu ya kwanza ya kiroho ambayo Yesu anataka kwa wale wanaotaka kuwa mojawapo ya ufumbuzi Wake au majibu Yake – kuwa chumvi ya dunia na nuru ya dunia – ni ile nidhamu ya usimamizi mzuri wa fedha na mali. Yesu anafundisha baadaye kwamba Mungu atazuia mali za kweli au baraka za kiroho – zisimfikie mwanafunzi ambaye si msimamizi wa mali aliye mwaminifu (ktk Luka 16:10, 11). Hii hufanya utoaji kuwa nidhamu mojawapo ya maana sana ya kiroho katika maisha ya mwanafunzi wa Yesu.

Nidhamu Ya Kiroho Ya Maombi

Yesu anataka mtazamo kama huo wakati anapofundisha wanafunzi Wake jinsi ya kuomba, hivi: "Na mnapoomba, msiwe kama wanafiki, kwa sababu wanapenda kuomba wakiwa wamesimama katika masinagogi na mitaani ili waonekane na watu. Nawaambia ukweli kwamba, wamekwisha pokea thawabu yao yote. Lakini ninyi mnapoomba, ingieni katika vyumba vya faragha, fungeni mlango na kumwomba Baba yenu asiyeonekana. Ndipo Baba yenu, aonaye yanayofanyika kwa siri, atakapowapa thawabu.

"Na mnapokuwa katika kuomba, msiseme-seme maneno bila utaratibu kama wapagani, kwa sababu wao wanafikiri kwamba watasikiwa kutokana na maneno yao mengi sana. Msiwe kama wao, kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua mnayohitaji kabla hamjamwomba.

"Basi, hivi ndivyo mnavyotakiwa kuomba:

> 'Baba yetu wa mbinguni, jina Lako litukuzwe, ufalme Wako uje, mapenzi Yako yafanyike duniani, kama huko mbinguni. Tupe leo chakula chetu cha kila siku. Tusamehe deni zetu, kama nasi tulivyowasamehe tunaowadai. Na usituongoze katika majaribu, bali tuokoe na yule mwovu. Kwa sababu, ufalme ni Wako, na nguvu na utukufu milele. Amina.'

“Kwa sababu, mkiwasamehe watu wanapowatendea dhambi, Baba yenu wa mbinguni atawasamehe na ninyi. Lakini msipowasamehe watu dhambi zao, Baba yenu hatawasemehe dhambi zenu hata ninyi” (6:5-15, TLR).

Kuomba si kuhubiri. Tunapoomba katika ibada ya watu wote, au tukiwa na wengine, lazima tukumbuke mafundisho haya ya Yesu, na kuhakikisha kwamba tunazungumza na Mungu. Yesu anatuonyesha jinsi ya kuhakikisha kwamba tunazungumza na Mungu wakati tunapoomba, anapotoa umuhimu wa kutosha kuonyesha kwamba anathamini zaidi maombi ya binafsi kuliko maombi ya pamoja na watu wengi. Anatushauri tuingie katika chumba cha faragha (au popote tunapoweza kuwa peke yetu), na kufunga mlango kwa sababu hakuna mwingine wa kujionyesha kwake hapo isipokuwa Mungu Mwenyewe.

Akiisha weka msingi kuhusu mwelekeo wa mwanafunzi Wake kuhusu maombi, Yesu anawafundisha jinsi ya kuomba. Anatupa maombi mfano ambayo yanapaswa kuitwa “Maombi ya Wanafunzi”. Mara nyingi yameitwa “Sala ya Bwana,” lakini hayatakiwi kuitwa hivyo kwa sababu Bwana hakuwahi kuomba sala hiyo. Ushauri Wake ni kwamba, “Basi, <u>ninyi</u> ombeni hivi.”

Ingawa hii ni sala, na ingawa maneno yake yanaonyesha kwamba inapaswa kuombwa kwa kushirikiana na watu wengine, kimsingi ni sala mfano, ambayo imekusudiwa kutufundisha jinsi ya kuomba. Luka anaonyesha Yesu akitoa sala hii kama itikio la ombi kutoka kwa mitume, kwamba, “Bwana! Tufundishe kuomba” (ktk Luka 11:1-4, TLR).

Kiini cha hii sala mfano ambayo Yesu alifundisha, ni zile sala tatu zinazomweka Mungu kwanza, na halafu yale maombi manne ya binafsi yanayofuata. Ombi la KiMungu ni ombi lenye kuwa na mambo mengi ya maana zaidi kwa Mungu. Ujumbe wa Biblia unakamilika kwa maneno mawili tu: “Mungu Kwanza”. Hizo sala tatu za mwanzo zinampa mwanafunzi changamoto kuomba kuhusu mambo yanayomhusu Mungu, kabla ya kuleta matatizo yetu binafsi kwa Mungu. Zile sala tatu zinazomweka Mungu kwanza ni: “Jina Lako litukuzwe, ufalme Wako uje,” na “mapenzi Yako yafanyike.”

Ombi binafsi ni ombi lenye mahitaji ya mwanafunzi kwa sehemu kubwa. Maombi manne ya binafsi ni haya: “Tupe siku ya leo chakula chetu, tusamehe madeni yetu kama tunavyowasamehe tunaowadai, usituongoze katika majaribu,” na “Tuokoe na yule Mwovu.”

Yesu anawafundisha wanafunzi Wake kuingia moja kwa moja katika uwepo wa Mungu na kumwita “Baba yetu!” Hilo lilikuwa wazo tofauti kabisa kwa wanafunzi waliosikia Yesu akitoa fundisho hilo. Wote walikuwa Wayahudi waliokuwa wamefundishwa maisha yao yote kumwona na kumwendea Mungu kama Mungu Mkuu na wa kutisha sana, ambaye angeweza kuendewa kupitia kwa nabii tu. Yesu hapa anamtambulisha Mungu binafsi – mwenye kuwajali watu – anayehusika katika kila sehemu ya mahitaji ya binafsi ya mwanafunzi Wake. Daudi pia alikuwa ameonyesha Mungu wa binafsi mwenye kujali watu wakati alipotamka hivi: “Bwana ni Mchungaji wangu” (ktk Zaburi ya 23).

Baada ya kumtaja Mungu kama Baba, kuna maombi matatu yenye kutufundisha kuomba mambo ya “Mungu kwanza” – Jina Lako, ufalme Wako, na mapenzi Yako. Jina la Mungu ndiyo kiini cha Yeye alivyo, na Yeye ni nani. Mwanafunzi anaomba hivi, kimsingi, “Mungu! Ninataka kuishi kwa namna ambayo wengine watajua na kukuheshimu Wewe kama ulivyo.”

Halafu tunatakiwa kuomba hivi: “Ufalme Wako uje”. Maana ya hili ni kwamba, Mungu ni Mfalme, na wanapomfanya Mfalme wao, wanakuwa sehemu ya ufalme Wake. Wanaomba hivi: “Baba, mimi sijengi ufalme wangu mwenyewe. Ninataka ufalme Wako utawale moyoni mwangu, nami nataka kuishi maisha yangu kama raia Wako mwaminifu kabisa.”

Ombi la tatu ni sawa na lile la pili: “Mapenzi Yako yafanyike hapa duniani, kama ilivyo huko mbinguni.” Anapokaribia kukamatwa na kusulubiwa, Yesu anatoa jasho la damu anapoomba hivi: “Ee Baba Yangu! Ikiwezekana, ruhusu kikombe hiki kiondoke kwangu. Lakini, si kama nitakavyo Mimi, bali kama Wewe utakavyo” (ktk Mathayo 26:39, TLR). Hiyo ndiyo tunayoweza kuiita “Sala ya Bwana” kwa sababu ni maombi aliyoomba Yesu. Yesu

hakuwafundisha wanafunzi Wake kuomba hii sala ya tatu tu. Yeye Mwenyewe alionyesha mfano wa kuomba hivyo alipokabiliwa na wakati mgumu katika maisha Yake.

Paulo anatuambia kwamba tunayo Hazina ya Kristo mfufuka katika vyombo vyetu vya udongo (yaani, katika miili yetu), ili iweze kudhihirika kwa kila mtu kwamba asili ya nguvu katika maisha yetu inatoka kwa Mungu, wala si kwetu. Msomi mmoja maarufu sana anaamini kwamba hili ombi la tatu linapaswa kuwa "katika dunia" badala ya "duniani". Anaamini kwamba Yesu alikuwa anafundisha kwamba tunapaswa kumwomba Baba yetu wa mbinguni kufanya mapenzi Yake katika vyombo vyetu vya udongo, kama ambavyo mapenzi Yake yanafanyika huko mbinguni. Bila shaka ni wazi kwamba, kama mapenzi ya Baba yatafanyika ndani yetu, basi mapenzi ya Baba yatafanyika duniani kupitia kwetu.

Hayo maombi matatu yanayomweka Mungu kwanza yanapaswa kutuma ujumbe kwa kila mwanafunzi wa Yesu kwamba, hawapaswi kuingia katika vyumba vyao vya maombi ya faragha, au katika maombi ya kuabudu hadharani, wakiwa na orodha ndefu ya "vitu vya kununua" ya matakwa yao na madai, kwa kusudi la kumtuma Mungu "dukani" kuwatafutia vitu vyao. Wakati wanapoomba, wanapaswa kuingia katika uwepo wa Mungu wakiwa na karatasi nyeupe tupu kabisa, na kumwomba Mungu awatume wao kufanya shughuli kwa ajili Yake. Katika maombi yao faraghani na hadharani, wanatakiwa kuwa kama askari wanaofika mbele ya mkuu wao – Jemadari wao na Mfalme – tayari kwa ajili ya kazi.

Yesu aliposhauri kwamba hayo maombi matatu ya Mungu kwanza yatangulie maombi ya mahitaji yetu, alikuwa anafundisha kwamba maombi si swala la kumshawishi Mungu kukubali kufanya mapenzi yetu. Kiini cha maombi ni kukubaliana na kulinganisha mapenzi yetu kwa mapenzi ya Mungu. Maombi si swala la kumfanya Mungu mshiriki mwenzetu katika mipango yetu. Kama Yesu alivyofundisha, kiini cha maombi ni Mungu kutufanya sisi washiriki Wake na kutuingiza katika mipango Yake.

Maombi Ya Binafsi

"Utupe chakula chetu cha siku ya leo …"

Lazima tuendelee kutazama mambo kupitia yale maombi ya "Mungu kwanza" hata tunapofikia kwenye ile sehemu ya "utupe" katika maombi haya tuliyofundishwa na Yesu. Yale maombi matatu ya "Mungu Kwanza" yanapaswa kutoa mwelekeo wa makusudi yetu tunapokwenda mbele ya Baba yetu wa mbinguni tukiwa na maombi yetu binafsi. Kwa nini tunataka Baba yetu wa mbinguni – Mungu – atupe sisi chakula cha kila siku, tena siku moja baada ya nyingine? Tunataka kumwomba baba yetu wa mbinguni aliye mkamilifu kabisa atupe chakula chetu cha kila siku kwa sababu tuna shauku sana ya kuona Yeye ni nani, na kwamba anaheshimiwa na kuabudiwa hapa duniani na kupitia kwetu.

Hii sala ya Yesu inatufundisha kwamba tunapaswa kuomba "leo" na "kila siku" tunapofikisha mahitaji yetu kama viumbe mbele ya Mwumbaji wetu na Baba yetu wa mbinguni. Ona jinsi Yesu anavyomalizia sura ya sita ya Mathayo kwa mkazo huo huo, hivi: "Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi kuhusu kesho, kwa sababu kesho itajisumbukia yenyewe. Kila siku ina matatizo yake ya kutosha" (ms. 34, TLR). Yaani kwa maneno mengine – ishi siku moja baada ya nyingine.

Katika hili ombi la kwanza la binafsi, Bwana anatumia mfano wa mkate kuwakilisha mahitaji yetu yote. Mkate ni mfano ambao haupaswi kuishia kwenye hitaji letu la chakula tu, bali unaoweza kutumika kwa ajili ya mahitaji yetu yote tuliyo nayo kama viumbe wa Mungu. Lazima tuwe na mkate kwa ajili ya kuhifadhi miili yetu kila siku, na ni lazima roho zetu na nafsi zetu zilishwe kwa mana kutoka mbinguni kila siku – kwa zamu.

"Tusamehe Deni Zetu Kama Tunavyowasamehe Tunaowadai"

Maombi matatu binafsi yanayofuata bila shaka yanahusu mahitaji yetu ya kiroho. Ombi la pili binafsi linahusu msamaha, na linafuatwa na ombi kuhusu kuongozwa na kukombolewa. Kanuni ya siku moja baada ya nyingine tunayojifunza katika ombi lile la chakula cha kila siku linapaswa kutumika katika haya maombi

matatu kwa ajili ya mahitaji yetu ya kiroho. Msamaha, uongozi na ukombozi ni mahitaji pia tuliyo nayo kila siku. Roho ya maombi hayo manne ya binafsi ni hii: "Tupe leo chakula chetu, pamoja na hitaji letu la kusamehewa, kuongozwa na kukombolewa."

"Usituongoze Kuingia Katika Majaribu …"

Kulingana na Yakobo, Mungu hajaribiwi na maovu, wala hamjaribu mtu yeyote (ktk Yakobo 1:13). Kutokana na mafundisho hayo, kwa nini basi Bwana wetu anatufundisha tumwombe Baba yetu Mungu wa mbinguni, asiyemjaribu mtu yeyote, kwamba, "Usituongoze kuingia katika majaribu?" Bila shaka roho ya ombi hili iko kwenye mafundisho ya jumla ya Maandiko yote kwamba sisi si nguzo imara wakati wa majaribu. Yesu alitathmini sawasawa hali yetu kama binadamu aliposema hivi: "Roho iko tayari, lakini mwili ni dhaifu" (ktk Mathayo 26:41, TLR).

Wakati Yesu alipokabiliana na hali ngumu kuliko zote maishani Mwake, aliwaomba mitume washirikiane Naye katika kuomba. Walipolala usingizi, aliwaamsha na kusema, "Mnatakiwa kuomba ili msiingie katika majaribu" (ktk Luka 22:46, TLR). Maana yake ni kama ifuatavyo: "Kama tu mngejua nguvu za Yule Mwovu na udhaifu wa miili yenu, mngekuwa macho mkiomba ili msije kukabiliana na majaribu."

Yesu anapotoa hili ombi binafsi la tatu, "Usituongoze kuingia katika majaribu," alikuwa sahihi kulingana na tathmini Yake ya hali yetu kama wanadamu – miili yetu – "asili ya kibinadamu bila msaada wa Mungu". Ni sawa pia kuomba hii sala ya tatu hivi: "Tuongoze, nasi hatutajikuta tunakabiliwa na majaribu ya kutenda dhambi."

" … Ila, Tuokoe Na Yule Mwovu."

Katika wimbo mmoja wa zamani sana, Martin Luther alituonya kwamba tunaye adui wa zamani wa kiroho ambaye hatutakii mema. Yeye anapinga vikali sana kila kitu ambacho Kristo anataka kufanya ndani yetu na kupitia kwetu. Ujanja na nguvu za Shetani ni mkubwa sana, na akiwa na chuki katili sana, hapa duniani hana mwenye kumweza. Kama tungetumaini nguvu zetu wenyewe, mashindano yetu yangeishia kushindwa tu, na kama tusingekuwa na

Mtu sahihi upande wetu, aliyechaguliwa na Mungu Mwenyewe. Pengine utauliza huyo ni nani? Huyo ni Kristo Yesu Mwenyewe!

Ombi hili la kukombolewa kutoka adui yetu wa zamani linapaswa kuombwa kila siku pia.

Ombi La Kumalizia Sehemu Ya Mungu Kwanza

"Kwa sababu, ufalme ni Wako, na nguvu na utukufu milele, amina."

Yesu alitufundisha kuanza na kumalizia maombi yetu kwa hoja ya Mungu kwanza, hivi: "Ufalme Wako uje," na, "Ufalme ni Wako." Wakati Yesu alipotoa ombi hili la kumalizia, alikuwa anatufundisha kumalizia maombi yetu kwa ahadi kubwa kwa Mungu kwamba matokeo na utukufu wa Yeye kujibu maombi yaliyoko katika sala hii mfano, daima vitakuwa Vyake.

Hitimisho

Maombi ambayo Yesu alitufundisha yanatupa changamoto ya kuhakikisha kwamba tunapoomba, tumwombe Mungu Baba. Hatufundishwi kumwomba Yesu au Roho Mtakatifu. Tunafundishwa kusema na Mungu kwa upekee sana kama Baba yetu mkamilifu, mwenye upendo, aliye mbinguni. Halafu tunatakiwa tuanze maombi yetu kwa sala tatu za Mungu Kwanza, ambazo ni: Jina Lako, ufalme Wako, na mapenzi Yako. Hizo sala tatu zinatakiwa kufuatiwa na maombi manne ya binafsi, hivi: Tupe, tusamehe, tuongoze, na tukomboe. Hatimaye, tunafundishwa kumalizia maombi yetu kwa kukiri kwamba: "Kwa kuwa nguvu za kujibu maombi yangu zitatoka Kwako siku zote, matokeo siku zote yatakuwa Yako, na utukufu siku zote utakuwa Wako. Na iwe hivyo!"

Nidhamu Ya Kufunga

Sawa na kutoa na kuomba, Yesu alifundisha kwamba taratibu ya kiroho ya kufunga lazima nayo ielekezwe juu (ms. 16-18). Ona kwamba Yesu hasemi, "Kama mtafunga". Anasema hivi: "Wakati mnapofunga". Aliwaambia wanafunzi Wake kwamba wakati wa kufunga, wasiwe na mwonekano wa njaa, kana kwamba wanasema,

“Ndiyo ninamalizia mfungo wa siku nne, nami nakaribia kuzimia!” Yesu aliwaambia wawe na sura ya kupendeza, iliyochangamka, wakati wakifunga.

Kama ambavyo kutoa kunatupa nafasi ya kupima uwajibikaji wetu kwa “Mungu Kwanza”, kufunga kunatupa nafasi ya kupima kiwango tunachothamini mambo ya kiroho kuliko ya kimwili, na huonyesha udhati katika maombi yetu. Kulingana na Yesu, kuna miujiza mingine ambayo inawezekana tu kwa kufunga na kuomba (ktk Mathayo 17:21).

Mambo Yenye Thamani Ya Juu Kwa Mwanafunzi

“Msijihifadhie vitu vya thamani hapa duniani, mahali ambapo nondo na kutu huviharibu na wezi kuvunja na kuiba. Jihifadhieni vitu vya thamani mbinguni, mahali ambapo nondo wala kutu haviwezi kufika na kuharibu, na mahali ambapo wezi hawawezi kuvunja wala kuiba. Kwa sababu, mahali vitu vyako vya thamani vilipo, ndipo na moyo wako utakapokuwa.

“Jicho ndiyo taa ya mwili. Kama macho yako ni mazuri, mwili wako wote utajaa nuru. Lakini kama macho yako ni mabaya, mwili wako wote utajaa giza. Basi, kama nuru iliyoko ndani yako ni giza, giza hilo ni kubwa mno!”

“Hakuna mtu awezaye kuwatumikia mabwana wawili. Anaweza kumchukia mmoja na kumpenda mwingine, au atakuwa mwaminifu kwa mmoja na kumdharau mwingine. Hamwezi kutumia Mungu pamoja na Fedha” (ktk Mathayo 6:24, TLR).

Sasa, Yesu anataka kuonyesha mambo ya thamani kwa mwanafunzi ambaye anaishi kulingana na zile hali za moyo alizofundisha. Kulingana na kamusi, kitu cha thamani ni: “Kile ambacho kinatamaniwa au kinachostahili kuthaminiwa kwa jinsi kilivyo.” Sababu moja ya wale watu waliokuwa chini ya mlima kuwa na matatizo mengi ni kwamba hawakuwa na thamani zilizo sahihi. Ili kuwa na ushawishi kama chumvi na nuru watakaporudi kwao, wanafunzi wa Yesu lazima wawe na thamani ambazo sasa anakwenda kuwafundisha.

Baada ya kutoa tamko la kuanza, ambalo ndani yake Yesu alifundisha kwamba hawapaswi kujimaliza kwa kutafuta vitu vya thamani au hazina ambazo zinapoteza thamani, au zinazoweza kuibiwa kutoka kwao, Yesu anataja mambo matatu muhimu sana kuhusu thamani. Cha kwanza anachotaja ni kiwango cha hali ya juu sana, ambacho wanafunzi Wake wanaweza kukitumia kupimia vitu wanavyothamini. "Kwa sababu, mahali vitu vyako vya thamani vilipo, ndipo na moyo wako utakapokuwa." Kwa maneno mengine anasema hivi, "Nionyeshe hazina zako ziko wapi, na utakuwa umenionyesha moyo wako, na vitu unavyothamini."

Anafuatisha hili kwa kutoa changamoto ambayo ni moja ya maswali muhimu sana yanayoweza kuulizwa na wanafunzi Wake – au hata kujibiwa nao. "Tunaonaje vitu?" Wakati Yesu anaposema, "Kama macho yako ni mazuri" (6:22), maana yake ni mtazamo wao. Thamani njema ndiyo tofauti kati ya mwili uliojaa nuru (furaha, usafi, baraka), na mwili uliojaa giza, au kutokuwa na furaha. Kama tulivyokwisha ona, wakati viongozi wa kidunia kama wale walioua mamilioni ya watu huko Uchina, Urusi na Ujerumani wanapokuwa na mtazamo mbaya, giza kubwa huifikia dunia yote.

Tamko Lake la tatu la ajabu sana kuhusu thamani, ni miongoni mwa maneno Yake magumu – wito kujitoa. Hawawezi kuwa na "mitazamo miwili" na kuwa wanafunzi Wake. Haiwezekani watumikie mabwana wawili – Mungu na fedha.

Maana Katika Maisha Binafsi

Lazima tuitikie hii changamoto ya Yesu. Je, tunajimaliza wenyewe kwa ajili ya mali au hazina za muda, au za milele? Kulingana na Yesu, swali hilo litajibiwa ikiwa tutatazama shughuli zetu za kila siku – tunayofanya kutwa n zima – na hali zetu za moyo, au, tunafikiri nini mchana kutwa; na wasiwasi wetu mchana kutwa; na tamaa zetu – yaani, tunachotaka mchana kutwa, na uaminifu wetu – tunamtumikia nani na nini mchana kutwa. Yesu hapa anatoa tamko lisilobadilika kwamba, mwanafunzi Wake hawezi kumtumikia Yeye kama Bwana na kutumikia tena kitu kingine au mtu mwingine. Kwa kuwa anatoa tamko hili katika mantiki ya fundisho hili juu ya mambo

ya thamani, kiwango Chake ni kwamba mwanafunzi hawezi kumtumikia Mungu na fedha.

Thamani Za Chumvi Na Nuru

"Kwa hiyo nawaambia hivi: Msiwe na wasiwasi kuhusu maisha yenu, mtakula nini au mtakunywa nini; wala kuhusu miili yenu, mtakachovaa. Kwani maisha si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Tazameni ndege wa angani, maana wao hawapandi wala kuvuna wala kukusanya na kuhifadhi katika ghala, lakini Baba yenu wa mbinguni anawalisha. Je, ninyi si wa thamani zaidi yao? Ni nani kati yenu ambaye, kwa kuwa na wasiwasi anaweza kujiongeza inchi moja katika urefu wake?

"Kwa nini basi mnakuwa na wasiwasi kuhusu nguo? Fikirini kuhusu maua ya shambani, jinsi yanavyoota: hayafanyi kazi wala hayashoni; lakini nawaambia kwamba, hata Sulemani mwenyewe katika utukufu wake wote, hakuvikwa nguo kama ua mojawapo. Sasa, kama Mungu anayavika hivyo majani ya shambani, ambayo leo yapo, na kesho yanatupwa katika tanuru la moto, atashindwa kuwavika zaidi ya hapo, ninyi wenye imani ndogo?" (ktk Mathayo 6:25-30, TLR).

Ingawa kuna mkazo mkubwa sana katika mistari hii kuhusu jinsi ya kushughulikia wasiwasi, kimsingi Yesu anachofundisha hapa ni mambo ya kuthamini. Ona maswali yasiyopungua ishirini anayouliza au kutaja kwa kupita, wakati thamani hizo zinapotolewa. Maswali kama: Mwili wako ni kitu gani? Nini thamani yako? Kwa nini kuwa na wasiwasi kuhusu mambo usiyoweza kutawala? Je, unamwamini Mungu anayewalisha ndege na kuyavika maua ya shambani, kwamba anaweza kukulisha na kukuvika wewe?

"Basi, msiwe na wasiwasi na kusema, 'Tutakula nini?' au 'Tutakunywa nini?' au 'Tutavaa nini?' Kwa sababu wapagani hukimbizana na hayo yote, na Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mnayahitaji. Ila, utafuteni kwanza ufalme Wake na haki Yake, na hayo mengine yote mtapewa vile vile.

“Kwa hiyo, msifadhaike kuhusu kesho, kwa sababu kesho itajisumbukia yenyewe. Kila siku ina matatizo yake ya kutosha” (ms. 31-34, TLR).

Neno lingine la mambo ya thamani ni mambo yenye umuhimu wa kwanza. Kutokana na mambo tunayothamini, kila mwanafunzi wa Yesu anapaswa kuwa na “lengo la mambo yenye umuhimu wa kwanza”, yanayozungukwa na mduara mmoja mweusi wenye miduara kumi na mbili inayounganika. Yesu anamalizia mafundisho Yake kuhusu vitu tunavyothamini kwa kutamka kwamba kiini cha malengo ya mwanafunzi Wake ya mambo muhimu, kiwe utawala wa Mungu katika mioyo yao. Miduara ile mingine yote inatakiwa kupewa umuhimu wa kwanza na Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, anapowaonyesha kilicho sahihi. Wao wanayo ahadi ya Yesu kwamba, mambo yote ambayo wanajaribiwa kuwa na wasiwasi juu yake mchana kutwa, yatatolewa na Baba yao wa mbinguni.

[USHUHUDA WA MWANDISHI: Nakushauri ukiri mambo hayo ya thamani, ya Yesu Kristo. Mke wangu na mimi tuliamua kukiri ahadi hiyo ya Yesu wakati tulipooana na kuanzisha kanisa. Yesu amekuwa mwaminifu kwa ahadi Yake kwetu tangu mwaka wa 1956. Mungu hajashindwa kutupa mahitaji yetu, Naye atahakikisha kwamba ahadi hiyo ya Yesu itatimizwa katika maisha yako kama utamfanya Yeye na yale yote anayotaka Yeye kuwa kitu muhimu cha kwanza katika maisha yako. MWISHO WA USHUHUDA]

Sura Ya Sita

"Mwaliko"

(Mathayo 7:1 – 27)

Katika hii sura ya mwisho ya Mahubiri ya Mlimani, tunasoma kwamba Yesu alimalizia mahubiri Yake kwa kutoa mwaliko kwa waliosikia kuamua kama watakuwa chumvi ya dunia na nuru, au kama watakuwa wasiofaa kwa lolote. Yesu alikuwa Mwalimu na Mhubiri wa hali ya juu sana aliyewahi kusikika hapa duniani. Anamalizia hii "Faragha ya Kwanza ya Kikristo" kwa kusema kwa wale waliosikiliza mafundisho Yake kwamba, "Kile tunachokiamini kweli, tunafanya. Mengine yote ni mazungumzo tu ya kidini – na hakuna mwenye kuhitaji maneno ya kidini!"

Yesu alikuwa amewafundisha wanafunzi Wake kutazama ndani na kutambua kwamba zile hali nane za moyo alizokuwa amefundisha zingewafanya wao kuwa chumvi na nuru kwa watu katika lile kundi kubwa, waliohitaji msaada. Pia aliwafundisha kutazama kando na kufanyia kazi hali hizo katika mahusiano yao. Hilo liliwapa changamoto sana kiasi kwamba walikuwa tayari kutazama juu na kupokea nguvu kutoka kwa Mungu – zile nidhamu za kiroho na mambo ya kuthamini – walizohitaji sana kama wangefikia mahali pa kutazama ndani na kando yao, kama ilivyowapasa.

Changamoto ya Yesu kwa sasa ni hii: "Mtafanya nini na kile mnachojua?" Mara kwa mara alitilia mkazo maana katika maisha, baada ya kutoa fundisho kuu kama hili. Baadaye, wakati anapowasafisha mitume miguu na kuwafundisha unyenyekevu, alitamka hivi: "Kama mnajua mambo haya, mtabarikiwa mkiyatenda!" Vile vile anauliza swali, "Mnawezaje kuniita Mimi 'Bwana, Bwana' na kutokufanya yale ninayosema?" (ktk Yohana 13:17; Luka 6:46, TLR).

Sasa atawahamasisha wale waliosikia mahubiri Yake kwa mashauri matatu, hivi: "Kabla hamjaondoka hapa mlimani, fanyeni

uamuzi wa kujitoa bila masharti yoyote, kutazama ndani, kando, na juu."

"Msihukumu, la sivyo ninyi pia mtahukumiwa. Kwa sababu, njia ile ile mnayotumia kuwahukumu wengine, itatumiwa kuwahukumu ninyi, na kipimo kile kile mnachotumia ninyi kupimia, mtapimiwa.

"Kwa nini unatazama kipande cha unga wa mbao kilicho katika jicho la ndugu yako, na kupuuza lile gogo katika jicho lako mwenyewe? Unawezaje kumwambia ndugu yako, 'Ngoja nitoe kipande hicho kilichoko katika jicho lako,' wakati wewe una gogo katika jicho lako mwenyewe? Ewe mnafiki! Toa kwanza gogo katika jicho lako mwenyewe, ndipo utakapoweza kuona vizuri kiasi cha kutoa kipande cha unga wa mbao katika jicho la ndugu yako.

"Msiwape mbwa vilivyo vitakatifu. Msiwatupie nguruwe lulu zenu. Mkifanya hivyo, wanaweza kuzikanyaga kwa miguu yao, halafu wawageukie na kuwararua vipande vipande" (7:1-6, TLR).

Yesu alikuwa mcheshi sana. Wakati mwingine alitumia vichekesho kufafanua na kuonyesha mfano wa kweli aliyokuwa anafundisha. Kwa mfano: Alisema hao viongozi wa dini walikuwa wanachuja mbu na kumeza ngamia (ktk Mathayo 23:24). Ili kukazia hoja Yake – kwamba wanafunzi Wake hawapaswi kuwa wenye kuhukumu kupita kiasi – Yesu anauliza maswali kadhaa. "Kwa nini unajaribu kutafuta kipande cha unga wa mbao katika macho ya wengine, wakati wewe mwenyewe una gogo katika jicho lako? Utawezaje kumsaidia mtu mwingine kutoa kipande hicho katika jicho lake, wakati wewe umesongwa na gogo kubwa katika jicho lako?"

Mtu mmoja alikwenda kumwona mchungaji wake. Alikuwa amebeba kabeji kichwani, na mayai mawili yaliyokaangwa pamoja na kipande cha nyama kwenye kila sikio. Mchungaji alipomwuliza – kwa mshangao mkubwa – "Vipi? Nikusaidieje?" Yule mtu alijibu, "Mchungaji, nataka kukwambia habari za ndugu yangu!" Kuna watu wengine ambao wanashughulika sana na matatizo ya watu wengine. Wakati mwingine wanatoa hukumu tu, nao wanalaumu daima watu

wengine kuhusu mambo, wakati ambapo ni wazi kabisa kwamba wenye shida ni wao.

Yesu anaeleza vizuri sana kuhusu watu hao kwa mfano huu wenye kuchekesha, lakini ulio wazi kabisa. Anauliza maswali mawili makubwa: “Kwa nini unafanya hivi?” Na, “Utafanikiwaje?” Kiini cha fundisho hili ni: jitoe kutazama ndani, uondoe gogo katika jicho lako ili uweze kuwasaidia watu wengine kuondoa vipande vya unga wa mbao katika macho yao.

Maneno yanayofuata kutoka kwa Yesu, hayachekeshi hata kidogo. Yesu alitoa maana ya mfano Wake wa kuchekesha, hivi: “Ewe mnafiki! Toa hilo gogo katika jicho lako, ndipo utakapoweza kuona vizuri kumsaidia ndugu yako kutoa kipande cha unga wa mbao kilicho katika jicho lake.” Kwa kuwa fundisho hili linaanza kwa tamko kwamba hatupaswi kuwahukumu wengine, watu wengi wanafikiri hiyo ndiyo kweli pekee aliyokuwa anafundisha Bwana Yesu hapa.

Ukweli ni kwamba alikuwa anafundisha kuwa, ikifikia kwenye matatizo ya mahusiano, mwanafunzi sharti ajiunge katika “Klabu ya Mimi Kwanza”. Mwanafunzi wa Yesu lazima amruhusu Mungu kushughulika na matatizo yake binafsi kabla ya kwenda kuwasaidia wengine katika matatizo yao. Kwa hiyo basi, wasiwahukumu wengine kwa ukali. Anachoshauri ni: “Jihukumu wewe kwanza, ndipo utakapoweza kuwasaidia wengine na matatizo yao. Jitoe kutazama ndani!”

Aliongezea fundisho hili kwamba mahusiano kati ya wanadamu yana pande mbili. Kipimo chochote utumiacho kwa wengine, watakitumia katika mahusiano na wewe. Huu ulikuwa mfano wa sokoni. Kama ulikuwa na mashaka kwamba mfanya biashara mwenzako hakuwa na kipimo sahihi, wakati wa wewe kumwuzia mazao yako, ungeweza kumwambia atumie kipimo alichotumia wakati uliponunua vitu kutoka kwake. Hapo, Yesu anamalizia mafundisho Yake kuhusu jinsi ya kuhusiana na mwanafunzi mwenzako.

Mafundisho Yake kuhusu lulu na nguruwe yanahitimisha mafundisho Yake kuhusu jinsi ya kuhusiana na wapinzani, watu

waovu, na maadui. Tunapaswa kuwafikia watu hao, lakini, yawezekana tukajipoteza wenyewe na lulu zetu, wakati watu hawajali tunachojaribu kuwapa. Hatupaswi kutokuwa na ufahamu, bali tuwe wasimamizi wenye hekima wa maisha yetu na huduma zetu.

Ushauri Wake wa pili ni kufanya uamuzi wa kujitoa kutazama juu: "Ombeni, nanyi mtapewa. Tafuteni na mtapata; pigeni hodi, na mlango utafunguliwa. Kwa sababu kila anayeomba hupokea, na kila anayetafuta hupata, na kila anayepiga hodi, atafunguliwa mlango.

"Nani kati yenu, ambaye mtoto wake wa kiume akimwomba mkate, atampa jiwe? Au kama ataomba samaki, atampa nyoka? Sasa, kama ninyi, ingawa ni waovu, mnajua jinsi ya kuwapa watoto wenu vitu vizuri, Baba yenu wa mbinguni si ndiyo kabisa? Atawapa wale wamwombao vitu vizuri!" (Mathayo 7:7-11, TLR).

Hii sura nzima ya sita imeandika ushauri wa Yesu kutazama juu na kupokea zile thamani na nidhamu za kiroho zitokazo kwa Mungu. Sasa anadai kujitoa kabisa, bila masharti yoyote, kwa ajili ya kujifunza na kufanyia kazi hizo nidhamu na thamani ambazo alifundisha alipotoa changamoto kwamba wanafunzi watazame juu.

Katika lugha ya Kiyunani, wakati uliopo ni tendo linaloendelea. Basi, hii mistari inaweza kusomeka hivi: "Ombeni, na mwendelee kuomba … kwa sababu yeye aombaye na kuendelea kuomba hupokea, n.k. n.k." Hoja ni kwamba, Yesu anawahimiza wanafunzi Wake kutazama juu daima, na kwa uvumilivu. Kutafuta ni kitu kinachoendelea, na kuomba na kupiga hodi ni vitu vya kudumu na ni utafutaji wenye nguvu. Yesu anawaita wanafunzi Wake wawe na bidii kwa habari ya Mungu!

Huu ushauri unamalizika kwa ahadi ya kusisimua sana kwamba kila mwenye kuomba, kutafuta na kubisha hodi kwa uvumilivu na juhudi atapokea, atapata na hatimaye kuona mlango uliofunguliwa, wenye kufika katika uwepo wa Mungu. Hiyo ahadi ya kushangaza sana inafuatwa na uhakikisho mzuri kabisa kwamba kama sisi tukiwa wanadamu wenye udhaifu na mapungufu mengi, tunawapa watoto wetu vitu vizuri, Baba yetu wa mbinguni mwenye

upendo na aliye mkamilifu sana bila shaka atatoa vitu vizuri kwa wale wanaomwomba.

Inashangaza mno kwamba watu wachache sana wanafundisha na kuhubiri huu mwaliko wa Yesu siku hizi. Inasikitisha pia kwamba, wanafunzi wachache kabisa wa Yesu huitikia mwaliko Wake huo wa kuwa wanafunzi wenye bidii katika Mungu.

Jambo la tatu ambalo Yesu anatoa kwa wanafunzi hao kabla hawajarudi kwenye mahusiano yanayowasubiri huko chini ya mlima ni mwito wa kufanya uamuzi kamili, usio na masharti yoyote, wa kutazama pembeni. “Basi, katika kila kitu, wafanyieni wengine kama ambavyo mngependa wao wawafanyie, maana hiyo ndiyo jumla ya Torati na Manabii” (Mathayo 7:12, TLR).

Yesu anamalizia mahubiri Yake kwa mstari huu, ambao unajulikana kama “Amri Iliyo Kuu” (au wengine wanaiita Ya Dhahabu). Ni fundisho kuu kuliko yote duniani, kuhusu mahusiano baina ya binadamu. Yesu anadai kwamba hii sentensi fupi sana inatimiza Torati na Manabii (Agano la Kale), au, Maandiko yote yaliyokuwepo wakati huo.

Msomi mmoja ameandika hivi: “Kama kawaida, kwa Yesu mambo muhimu ni yale mambo rahisi, na mambo yaliyo dhahiri ndiyo mambo muhimu.” Anachofundisha hapa ni hiki: “Mchague mtu yeyote katika lile kundi pale chini ya mlima. Jiweke katika nafasi yake. Kama ungekuwa huyo, ungetaka mwanafunzi wa Yesu akufanyie nini? Ukipata jibu la swali hilo, fanya basi – chochote kile – fanya! Hilo ndilo fundisho zima la Biblia kuhusu swala la mahusiano baina ya watu.”

Hebu tia katika vitendo fundisho hili – kwa mwenzako wa ndoa, kwa watoto wako, kwa wazazi wako, au kwa ndugu na dada zako katika Kristo. Fanyia kazi fundisho hilo kwa watu wa kabila au taifa lingine. Linakuwa Amri Kuu kwa ajili ya mahusiano kikabila, katika ndoa na jamaa na jumuiya ya kiroho. Hakikisha pia kwamba unalifanyia kazi kwa wapinzani wako na adui zako.

Labda maana halisi katika maisha ya fundisho hili moyoni mwa Yesu ni kulifanyia kazi kwa watu wasiojua chochote kuhusu Kristo, na wokovu. Hapo inakuwa Amri Kuu ya utume na uinjilisti.

Mwaliko Mkuu

Baada ya kutoa miito Yake mitatu kwa wanafunzi kwamba wajitoe, yenye kumalizika na Amri Kuu, sasa Yesu anatoa mwaliko kwa maneno magumu. Hakuwahi kuwaalika watu wafike kupata kitu pasipo gharama yoyote. Huu haukuwa mwaliko watu waje kuokoka, bali ni changamoto Yake ili watu wawe majibu na ufumbuzi wa Yesu, na kuifikia dunia kwa ajili Yake.

Hii kawaida ya kutoa mwaliko wenye kuwafikisha wale waliokuwa wanasikiliza mahubiri au mafundisho kwenye mahali pa kuamua na kujitoa inaanzia kwa Musa na manabii (ktk Kumbukumbu 30:19, 20). Kutoa mwaliko kilikuwa kitu muhimu na cha tofauti sana katika huduma ya Yesu Kristo. Wakati faragha hii ilipoandaliwa, changamoto ilikuwa hii: “Je, wewe ni sehemu ya tatizo, au utakuwa sehemu ya ufumbuzi? Je, uko na makundi kule chini ya mlima, au uko juu ya mlima pamoja na Yesu?”

Lakini mwisho wa mafundisho, wale wanaokiri kuwa wanafunzi wa Yesu, na ambao wanadai kwamba watakuwa majibu au ufumbuzi Wake, wanasikia mwaliko wa kushangaza. Kumbuka, wote waliosikia mwaliko huu walidai kuwa waamini. Huu ni mwaliko unaotolewa kwa wanafunzi pale juu ya mlima. Jambo kuu katika mwaliko huo ni hili: Wewe ni mwanafunzi wa namna gani?

Mwaliko wenyewe ni huu: “Ingia kupitia mlango mwembamba; kwa sababu kuna mlango na njia pana iongozayo kwenye uharibifu, na kuna wengi sana wanaoifuata. Kwa sababu, mlango ni mwembamba na njia iendayo uzimani ni ngumu, na ni wachache sana wanaoipata” (ms. 13, 14, TLR).

Mambo ni mawili. Katika mwaliko huu, Yesu atasema kwamba kuna aina mbili za wanafunzi. Katika sehemu hii ya mwaliko, anasema kuna wengi na kuna wachache. Wale wengi hufikiri kwamba kuna njia rahisi ya kuwa ufumbuzi, ya kuwa jibu, ya kuwa chumvi na nuru. Lakini hawafanyiki majibu wala ufumbuzi. Wao si chumvi yenye ladha ya chumvi, na si nuru inayong’aa sana, ila, wanadai kuwa hivyo. Yesu anasema hivi, kimsingi: “Mkitazama yanayowapata wengi wanaofuata njia isiyokuwa na upinzani sana na

kufikiri kwamba kuna njia rahisi ya kufanyika sehemu ya jibu Langu na ufumbuzi, mtaamua kwamba hamtaki kuwa mmoja katika wengi.

"Lakini tena, kuna wachache. Wao wanajua kwamba hakuna njia rahisi. Wale wengi wanaamini kwamba inaanzia kwenye mlango mpana ambao unafuatiwa na barabara pana, iliyokaa vizuri, ila inaelekea kwenye uharibifu. Wachache wanajua kwamba lango ni dogo na njia inayofuata baada ya lango hilo ni nyembamba, ngumu na yenye kuhitaji nidhamu sana. Lakini njia hiyo huelekeza uzimani. Ni wachache tu wanaoipata. Changamoto ni hii: Je, wewe ni mmoja wa wengi, au wa wachache?"

Halafu Yesu anataja mambo mawili mengine. "Iweni macho kuhusu manabii wa uongo, wanaowajia wakiwa wamevaa mavazi ya kondoo, lakini ndani ni mbweha wakali sana. Mtawajua kwa matunda yao. Je, watu hukusanya zabibu kutoka kwenye miti ya miiba, au tini kutoka kwenye michongoma? Vivyo hivyo, kila mti mzuri huzaa matunda mazuri, lakini mti mbaya huzaa matunda mabaya. Mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri. Kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa katika moto. Kwa hiyo, mtawajua kwa matunda yao" (ms. 15-20, TLR).

Mwaliko wenye maneno mazito unaendelea. "Je, wewe ni mwanafunzi wa uongo au wa kweli?" Yesu alifundisha Mfano wa Ngano na Magugu, na ndani yake alitabiri kabisa kwamba ufalme wake (au Kanisa) utakuwa mchanganyiko wa walio kweli na waongo (Mathayo 13:24-30). Hata alifundisha kwamba hatutaweza kuwatofautisha. Basi, tusishangae kusikia mwaliko Wake ukionyesha uwezekano wa makundi hayo mawili – kuwepo kwa mwanafunzi wa kweli na wa uongo.

Anarudia ule mfano wa sheria ya kawaida katika dunia ya kiroho anapotamka kwamba tunaweza kutambua tofauti katika maisha yetu na katika maisha ya wengine, hivi: "Kila mti mzuri huzaa matunda mazuri. Miti mibaya huzaa matunda mabaya. Mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri." Vivyo hivyo pia, "Mti mzuri hauwezi kuzaa matunda mabaya." Changamoto ni hii: Wewe

ni mti mzuri au mbaya? Je, wewe ni mwanafunzi wa kweli au wa uongo?"

Sikiliza na hili: "Si kila mtu anayeniambia, 'Bwana, Bwana,' ataingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yule afanyaye mapenzi ya Baba Yangu aliye mbinguni. Wengi siku ile wataniambia, 'Bwana, Bwana, hatujatabiri kwa jina Lako, na kutoa pepo kwa jina Lako, na kufanya maajabu mengi kwa jina Lako? Ndipo na Mimi nitakapowaambia, 'Sikuwajua; ondokeni kwangu, ninyi mnaotenda uasi'!" (ktk Mathayo 7:21-23, TLR).

Hayo ni miongoni mwa maneno mazito sana katika Agano Jipya. Wanafunzi watatumia maneno matatu kutoa tathmini ya maisha na huduma zao walipokuwa wanamfuata Yesu. "Matendo mengi ya ajabu sana!" Ndipo Yesu naye atakapotumia maneno mawili kuwapa uamuzi na hukumu Yake kuhusu maisha yao na huduma: "Watenda uasi!"

Huu mwaliko wa Yesu ambao ni mgumu sana unataja uwezekano wa tatu, hivi: "Je, wewe ni mmoja wa wale wanafunzi wa Yesu wanaosema tu, au ni mmoja katika wale wanaofanya mapenzi ya Baba?"

Hii inamwongoza Yesu kwenye kumalizia kwa hali ya juu kwa mahubiri Yake maarufu. "Kwa hiyo, kila anayesikia maneno Yangu haya na kuyafanya, nitamfananisha na mtu mwenye hekima aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba. Mvua ikashuka, gharika ikaja, na upepo ukavuma na kuipiga nyumba hiyo; wala haikuanguka, kwa sababu ilikuwa na msingi wake juu ya mwamba. Sasa, kila asikiaye haya maneno Yangu na kutoyafanya, ni sawa na mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga. Mvua ikanyesha, gharika ikaja, na upepo ukavuma na kuipiga hiyo nyumba, nayo ikaanguka. Na anguko lake lilikuwa kubwa" (ms. 24-27, TLR).

Hayo maneno ya Yesu ya kumalizia yanaendeleza ule mwaliko Wake wenye kiini cha "wanaosema, na wanaofanya". Changamoto ya mwisho ni kwamba, kama mwanafunzi amesikia mafundisho haya na asiyafanyie kazi kabisa, hana msingi kwa ajili ya maisha yake au kwa ajili ya ukiri wake wa imani. Kama

wakiyafanyia kazi hayo waliyoyasikia, basi maisha yao, na imani yao pia, vimejengwa kwenye msingi imara.

Ukipewa karatasi na rangi za kuchorea, na uwe mchoraji stadi, halafu uambiwe chora picha ya "maisha", ungechora kitu gani? Pengine vijana wangechora kitu cha ajabu kama vile kijana akistarehe. Wazazi wao wangechora kitu thabiti ambacho kingeonyesha maisha magumu waliyoishi.

Yesu hakuwa na mtazamo rahisi, wala hakuwa na mtazamo kinyume. Yeye alikuwa na mtazamo halisi. Alifundisha kwamba maisha ni dhoruba. Hakuna asiyepatikana na dhoruba za maisha. Hizi dhoruba zilipiga hizo nyumba zote mbili. Lakini maisha yaliyojengwa kwenye kutii mafundisho Yake hustahimili dhoruba, na maisha yenye kusikiliza tu mafundisho Yake bila ya kuyatii hayastahimili. Maisha hayo huanguka, na anguko lake ni kubwa sana! Mahubiri hayo yanamalizika kwa changamoto tena: "Wewe ni mwanafunzi aina gani?"

Maneno ya mwisho tunayosoma ni itikio la watu ambao hawakuhudhuria, lakini walikuwa kwenye miinuko iliyokuwa karibu na kilele cha ule mlima, wakaona mtindo wa kufundisha kwa Yesu. "Baada ya Yesu kumaliza kusema hayo, watu walishangazwa na mafundisho Yake, kwa sababu alifundisha kama mtu mwenye mamlaka, wala si kama waalimu wao wa Torati" (ms. 28, 29, TLR).

Hitimisho

Yesu anakualika wewe, kama alivyowaalika wale wanafunzi Wake, uwe sehemu ya majibu Yake kwa makundi ya watu wanaotanga-tanga katika giza lisilo na matumaini. Soma hizo sura tena na tena na umwombe Mungu akusaidie ili usielewe tu, bali uishi na kutii mafundisho Yake. Halafu, "Omba, nawe utapewa. Tafuta, na utapata. Piga hodi, na mlango utafunguliwa" (Mathayo 7:7).

Ni maombi yetu kwamba Mungu ametumia mafundisho haya kukusaidia na kukutia moyo ili uwe nuru inayong'aa vizuri mahali ambapo Mungu amekuweka.